

**Wamkataa** mbunge mbele ya Makonda

UKURASA 3

**Hamas** wakiri makosa uvamizi nchini Israel

UKURASA 19



**Donald** Trump anyanyuka kisiasa uchaguzi USA

UKURASA 19

**NINA MBINU YA KUFUNGA KILA MCHEZO**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumanne Januari 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581564

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz

www.ippmedia.com

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


MKUU WA MAJESHI ASEMA...

# Kuna wakimbizi viongozi serikalini

• **Rais** Samia aahidi kulifanyia kazi... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ya Wananchi wa Tanzania Jenerali Jacob John Mkunda wakati wa mkutano wa CDF na Makamanda kwa mwaka 2023 ambao ulifanyika Lugalo Jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 4

## NDEGE YA MIZIGO ATCL KUTUA GUANGZHOU

SHIRIKA la Ndege la ATCL, limesema kutokana na mahitaji makubwa ya usafirishaji wa shehena kati ya China...

UKURASA WA 22

## KOCHA ZAMBIA ASIKITISHWA NA SARE



KOCHA Mkuu wa Zambia, Avram Grant amesikitishwa na sare yao dhidi ya Tanzania kwenye...

U KURASA WA 22

## KOCHA WA MOROCCO AKUBALI KUBEBA LAWAMA DR CONGO

KOCHA wa Morocco, Walid Regragui, amesema lawama zote amezibeba yeye kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya DR Congo...

## Mbowe: Polisi wameridhia maandamano ya CHADEMA

UKURASA 3



Wafanyakazi wakiendelea na kazi ya kuondoa magogo jana ambayo yalikwama katikati ya barabara ya Morogoro eneo la Jangwani jijini Dar es Salaam na kuzia magari baada ya kusombwa na mvua iliyonyesha juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**


## Asasi 200 zakataa uteuzi viti maalum

UKURASA 2

**MICHEZO** TAIFA STARS YAAPA KUFA NA DR CONGO UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati,Dk. Doto Biteko akisalimiana na Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa China, Liu Guozhong ambaye amewasili nchini kwa ziara ya siku tatu. **PICHA: TERESIA MHAGAMA**

MKUU WA MAJESHI ASEMA...

# Kuna wakimbizi viongozi serikalini

**Na Jenifer Gilla**

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi (CDF), Jenerali Jacob Mkunda amesema baadhi ya wakimbizi na waomba hifadhi nchini wameajiriwa na wengine kuteuliwa katika nafasi za kufanya uamuzi serikalini.

Ameshauri serikali kufanya utaratibu wa kuwarudisha watu hao nchini kwao kwa kuwa kuendelea kuwapo kwao nchini kwa muda mrefu kunaiweka nchi katika hali ya hatari.

Jenerali Mkunda alimweleza hayo Amiri Jeshi Mkuu, Rais Samia Suluhu Hassan jana Dar es Salaam wakati akifungua Mkutano wa Saba wa CDF na Makamanda.

Alisema kuanzia Januari Mosi hadi Desemba 31, mwaka jana, jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi 138,149 walipokewa nchini. Ni hatari kubwa, hasa katika mikoa ya magharibi kwa kuwa ndiko waliko waliokaa kwa muda mrefu.

Alisema wakimbizi hao wanaotoka kwenye nchi za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, hutumia mbinu mbalimbali kuhakikisha uzao wao unapata uraia wa Tanzania bila kufuata sheria.

"Kutokana na mahojiano ya awali imebainika kwamba waomba hifadhi wengi wamekuja Tanzania kwa sababu za kiuchumi, kwani Tanzania imebainika kuwa na fursa nyingi za kiuchumi kuliko nchi walizotoka.

"Hata hivyo, sababu zinazowafanya wakimbie nchi zao zinawakosesha sifa ya kupewa hadhi ya ukimbizi," alisema.

Jenerali Mkunda pia alisema hali ya ulinzi na usalama kwa sasa ni shwari licha ya kuwapo matukio ya kigaidi na itikadi kali na vijana wa kitanzania kati ya miaka 15 hadi 35 kujiunga na makundi ya kigaidi katika nchi za DR Congo, Msumbiji na Somalia.

Alisema tishio lingine la usalama wa nchi ni dawa za kulevya, matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii na ongezeko la wahamiaji haramu. Hata hivyo, Jenerali Mkunda alisema jeshi limendelea kuyadhibiti kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama.

Mkuu huyo wa Majeshi alishauri serikali kuimarisha barabara za ulinzi katika maeneo ya mipaka ya nchi ili kudhibiti vitendo vya uvunjifu wa amani kutoka kwa magaidi wa nchi wanazopakana nazo.

Vilevile, aliiomba serikali kuijengea uwezo Suma JKT kitengo cha ujenzi ili wajikite katika ujenzi wa kitaifa.

**RAIS SAMIA**

Akijibu ombi kuhusu wakimbizi, Rais Samia alisema serikali imelipokea na itaanza mchakato wa kuwachambua wakimbizi hao na kuzungumza na nchi wanazotoka ili kuandaa utaratibu wa kuwarudisha.

Alisema serikali pia itafanyia kazi ushauri uliotolewa wa kuimarisha barabara za ulinzi zilizoko mipakani ili kuimarisha hali ya usalama na nchi jirani.

Alishauri jeshi hilo kujiimarisha na kujiongezea uwezo ili kwenda sawa na maendeleo ya teknolojia hata kukabiliana na mbinu mpya za kigaidi.

Alilihakikishia jeshi kuwa serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufanya kazi ikiwamo kuwapatia mafunzo, rasilimali watu na fedha na zana ili watimize wajibu wake ipasavyo.

"Jinsi uchumi unavyokuwa, ndivyo vyombo vyetu vya usalama vinavyoimarika. Kwahiyo, tujitahidi kuweka ulinzi na usalama ili tupate nguvu zaidi ya kuvipa nguvu vyombo vyetu," alisema.

Alilishauri kutumia mkutano huo kujitafakari hali yake kikanda na kimataifa na kuandaa mikakati ya kuliboresha zaidi kwa miaka 60 ijayo, ili kuendeleza kazi nzuri ya kuimarisha amani na usalama wa nchi kwa manufaa ya watanzania.

**PICHA YA GWANDA**

Rais Samia pia alifurahia zawadi ya picha yake aliyokuwa amevaa sare za jeshi hilo, akisema kuwa siku alipovaa mavazi hayo, ilibadilisha mitazamo ya baadhi ya watu kuwa hatoweza kuwa Amiri Jeshi Mkuu kwa kuwa ni mwanamke anayevaa hijabu.

"Sasa siku mlionivisha kombati hii, watu walijua kwamba kila kitu kinawezekana, Na siku ile ndio mlijenga imani ya watanzania juu ya wanawake, ninawashukuru sana," alisema.

Rais Samia pia aliliomba lijiandae kuimarisha amani na usalama katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani kwa kukabiliana na hali yoyote ya kuhatarisha amani itakayojitokeza katika kipindi hicho.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax alisema kuwapo Rais Samia katika mkutano huo kutawaongeza ari na hamasa wajumbe ambao ni watendaji katika kamandi, vyuo na vikosi mbalimbali katika jeshi hilo.

**MAONI YA WADAU**

Rais wa Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), Harold Sungusia, alisema kinachosababisha wakimbizi kuajiriwa serikalini ni mifumo mibovu ya kutambua na kutofautisha raia na asiye raia wa nchi na kuwapa uhalali wasio husika.

Alitaja sababu nyingine kuwa ni changamoto za kibinadamu ikiwamo rushwa katika mamlaka zinazohusika na usalama wa raia mali zao ambao baadhi yao hushawishika kutoa vitambulisho kwa wasio raia.

Alishauri mamlaka zinazohusika na mifumo ya usimamizi wa utambuzi wa raia wafanye kazi zao kwa weledi ili kudhibiti masuala hayo kwa sababu ni hatari kuwa na viongozi ambao sio watanzania.

# Asasi 200 zakataa uteuzi viti maalum

**Na Elizabeth Zaya**

MTANDAO wa Wanawake Katiba, Uchaguzi na Uongozi (WFT) unaojumuisha mashirika na asasi za kiraia 200, umependekeza kuondolewa kwa viti maalum vya ubunge na udiwani, badala yake kuwapo mabadiliko ya kisheria yatakayowezesha kufikia uwakilishi wa 50/50 kwa njia ya majimbo ya uchaguzi.

Umesema ni vyema wanawake wapigiwe kura na wapigakura wote badala ya kuviacha vyama vya siasa kutumia au kugeuza haki za wanawake kwenye kuteuliwa kama ni jambo la hiari au hisani.

Mtandao huo umetaka mapendekezo hayo yaingizwe kwenye miswada ya: Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani; Sheria ya Vyama vya Siasa; na wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2023 kabla ya kuiwasilisha bungeni na kusomwa kwa mara ya pili.

Wakitoa tamko hilo mbele ya waandishi wa habari jana, wajumbe kutoka kwenye mtandao huo, walisema kipindi chote ambacho wanawake wamekuwa wakipewa viti maalum, kilikuwa ni kama cha kujifunza lakini imetosha kujifunza na sasa wanatakiwa wasimame majimboni 50/50 kuwania nafasi hizo na kuonesha uwezo wao kamili.

Walisema kwamba viti hivyo maaalum pamoja na kwamba wao ndio pia walipambana kuvidai kwa ajili ya kuongeza idadi ya uwakilishi wa sauti za wanawake, sasa vimekuwa vinatumika na kuchukuliwa kwa mtazamo hasi ikiwamo kurithishana, hisani na kugubikwa na rushwa ya ngono na hivyo kushindwa kuweka watu sahihi na wenye uwezo wa kuwakilisha wanananchi.

Baadhi ya walioshiriki katika kuandaa tamko hilo ni Mkurugenzi mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Hellen Kijo Bisimba, Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Annanilea Nkya, Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania, Gema Akilimali, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Msichana Initiative, Rebeca Gyumi.

Akisoma tamko hilo, Kaimu Mwenyekiti wa Mtandao huo, Mary Ndaro, alisema kinachotakiwa kufanyika ni kuweka mfumo wa wazi, huru na salama wa kuwezesha wa wanawake kutumia haki zao za msingi za kuchagua na kushindana.

Alisema mfumo wa sasa wa utoaji wa viti maalum, unakinzana na azma ya kujenga demokrasia shirikishi kwa mrengo wa jinsia kwa sababu umejenga daraja na ubaguzi kati ya wawakilishi wa majimbo katika uteuzi za nafasi mbalimbali pamoja na stahiki tofauti, ikiwa ni pamoja na kutoshika au kuteuliwa katika nafasi za Waziri Mkuu, Spika, kuongoza Baraza la Madiwani na kutokustahili mfuko wa jimbo.

Pia alisema mfumo huo unawanyima wanawake ushiriki katika kupigiwa kura na raia wote na kuviacha vyama vya siasa kuteua wawakilishi hao wa viti maalumu kwa ajili ya maslahi ya vyama na kwa kutumia mifumo ya uteuzi ambayo haina uwazi, kuwaweka katika hatari ya kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji wakati wa michakato kwenye vyama vyao ikiwa ni pamoja na rushwa ya ngono.

Alisema wanataka sheria iwajibishe vyama vya siasa kuzingatia misingi wa usawa katika uteuzi wa wote wanaowania nafasi kwenye uchaguzi wa udiwani na ubunge pamoja na uteuzi kwenye ushiriki wa uongozi kwenye vyama vyao.

"Tukumbuke kwamba vyama vya siasa vina wajibu mkubwa wa kuwezesha mfumo wa ushiriki wa wanawake kwenye meza za uamuzi. Vyenyewe ndivyo vina uwezo mkubwa wa kufunga au kufungua milango ya nani aingie kwenye kinyang`anyiro cha uchaguzi, nani ashinde na nani afungiwe milango," alisema Ndaro.

Jambo jingine walipendekeza kwamba muswada wa uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani ubainishe usawa wa jinsia wa 50/50 kwa kuvitaka vyama vya siasa vyote vyenye nia ya kushindania nafasi ya urais wa jamhuri, viteuwe wagombea wawili, mgombea urais na makamu wake.

# Mbowe: Polisi wameridhia maandamano ya CHADEMA

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limeruhusu maandamano yao ya amani yatakayofanyika kesho.

Kwa mujibu wa taarifa iliyoandikwa kwenye mtandao wa X wa Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, hatua hiyo imefikiwa baada ya mazungumzo ya jeshi hilo na chama hicho.

"Timu yetu ya chama ikiongozwa na Naibu Katibu Mkuu Bara, Benson Kigaila, imekuwa na kikao na Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, ACP Jumanne Muliro, makubaliano yamefikiwa kuwa maandamano yaendelee kama yalivyopangwa. Ninalipongeza Jeshi la Polisi kwa busara hii.," aliandika Mbowe.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika alisema maandalizi na maandamano ya amani ni kushinikiza kuondolewa miswada mitatu ya sheria za uchaguzi na ugumu wa maisha yanaendelea vizuri.

Miswada hiyo ni ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa ya Mwaka 2023.

Akizungumza na waandishi wa habari, Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA, Benson Kigaila, alisema maandalizi ya maandamano hayo yamekamilika kwa asilimia 100.

Alisema waliandika barua kwa Jeshi la Polisi, Januari 17, mwaka huu siku saba kabla ya maandamano, lengo likiwa ni kulipa muda wa kutosha ili washauriane na wafanye maandamano kwa amani.

Alisema juzi Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, aliwapigia simu na kuwaalika kukutana naye jana saa tano asubuhi kujadili suala hilo.

Alilipongeza jeshi hilo kuwa hatua hiyo ya kuonyesha serikali ilivyobadilika na kuwa na weledi tofauti na miaka ya nyuma ambayo walikuwa wakichukulia vyama vya siasa havijui chochote kuhusu usalama.

"Na sisi kama chama tutawapa ushirikiano wote kuhakikisha maandamano hayo yawe na usalama na baada ya maandamano tutafanya kikao cha tathmini," alisema.

Kigaila alisema wanawataarifu Watanzania kuwa wasiwe na wasiwasi wanapoona jeshi la polisi katika maandamano kwa kuwa halitatawanya watu bali kudumisha usalama.

Alisema licha ya maandamano hayo kuandaliwa na CHADEMA, lakini wanawaalika wananchi wote wapenda maendeleo ya nchi wawaunge mkono kuidhinisha serikali kufanya mabadiliko katika miswada hiyo.

Alisema maandamano hayo ni endelevu na yatafanyika nchi nzima kwa kuwa lengo ni kuitaka serikali kuja na mikakati ya kupunguza ugumu wa maisha kuiondoa miswada hiyo bungeni.

**MAONI YA WADAU**

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alipongeza hatua hiyo akiamini kwamba huenda ni utekelezaji wa ahadi ya Rais ya kuimarisha demokrasia nchini.

"Ni hatua kubwa kwa kweli kwa nchi yetu na nafikiri ni ahadi aliyoitoa Rais ya kufungua na kuimarisha Demokrasia, Uhuru wa kujieleza na watu kutoa maoni, tunapongeza kwa hilo kwa kweli," alisema Ado.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema hiyo ni dalili njema inayoonyesha kuwa demokrasia nchini imeanza kufunguka baada ya miaka mingi maandamano hayo kuwa yanazuiwa.

"Maandamano ni sehemu ya mtu au kikundi cha watu kutoa maoni yao ilimradi yasiwe ya kuleta vurugu na Jeshi la Polisi lenyewe linapaswa kupewa taarifa na kuyalinda maandamano siyo kupiga marufuku," alisema Henga.

***Imeandikwa na Elizabeth Zaya na Jenifer Gilla**

# Wamkataa mbunge mbele ya Makonda

**Na Beatrice Shayo,**
aliyekuwa SAME

WANANCHI wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro wamemkataa mbunge wao, David Mathayo kwa madai hakuna anachokifanya kuwaletea maendeleo na haonekani jimboni wala bungeni.

Wananchi hao walitoa malalamiko yao jana wilayani hapo mkoani Kilimanjaro wakati wa ziara ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, wakieleza mbunge huyo amewasahau wananchi wake katika maendeleo.

Raphael Mruta, mkazi wa Same, alisema changamoto kubwa ni kukosekana kwa maeneo na kuwapo siasa chafu.

Alisema kurudi kwa Jimbo la Same CCM ni watakapokuwa na siasa safi kwa kuwa wana mbunge ambaye haonekani bungeni na jimboni.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, Makonda aliwahoji wananchi; "Wangapi wanasema mbunge haonekani jimboni wala bungeni," wananchi hao walinyoosha mikono huku wakishangilia na kusema aondoke.

Makonda alisema maelekezo ya Mwenyekiti wao taifa ambaye ni Rais Samia Suluhu Hassan, yapo wazi Mathayo na wabunge wote wa CCM, madiwani na wawakilishi watakapokaa kwenye kikao cha Halmashauri Kuu taifa kujadili majina yao wataangalia sifa kubwa mbili.

Alizitaja sifa hizo kuwa amefanya nini kwenye jimbo lake kwa niaba ya wananchi waliomchagua na wataangalia ana mchango gani katika chama chake.

"Kama hafanyi kazi kwa wananchi, wananchi wana kero haangaiki huyo hatarudi kwa hiyo kama kaka yangu Mathayo ni miongoni mwa wasiofanya kazi nawahakikishia hatarudi," alisema Makonda na kuongeza:

"Kitakachomrudisha ni utendaji wake wa kazi, inaonekana bado hujakubalika vizuri kwenye jimbo lako la Same na hatutaki wagombee siku za mwisho wanakuja na briefcase kugawa pesa, wananunua kamati za siasa, wananunua wajumbe halafu mwishoni tunapoteza uhalali kwa wananchi," alionya.

Kadhalika, jukumu lake ni kuongeza idadi ya uhai wa chama na wanachama na kuhakikisha wanapata ushindi unaotokana na utendaji wao wa kazi.

Akizungumza katika hadhara hiyo, Mathayo alisema wana changamoto katika kijiji cha Hedaru wanaunganishiwa umeme kwa Sh. 320,000 wakati vijiji vingine wanachangia Sh. 27,000.

Alisema tatizo lingine ni wakati wa ukame wanyama wanaotoka Hifadhi ya Mkomanzi wanawaumiza wananchi, nyumba zao na mashamba yanashambuliwa na wanyama na inapotokea fidia wanasumbuliwa.

Alisema fidia inayolipwa ni kidogo hata mtu akiuawa na tembo analipwa pesa ndogo wakati tembo mmoja akiuliwa analipwa hadi Sh. milioni 40.

"Tufike mahala binadamu awe ni muhimu kuliko mnyama tunayemsimamia tembo akiuliwa fidia analipwa hadi Sh. milioni 40," alisema Mathayo.

## IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
## DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY
## AT DAR ES SALAAM
## CIVIL CASE NO. 157 OF 2022
## LONGINO LAZARO @ KASONTA

...............

**PLAINTIFF**

**VERSUS**

**MOHAMED SUMAR......DEFENDANT**

**TO:**

**MOHAMED SUMAR,**
**P.O.Box,**
**DAR ES SALAAM**

**WHEREAS,** the above mentioned case has been fixed for mention on 20th day of February, 2024 at 9:00AM before Hon. A. A. MBAGWA –Judge you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day aforementioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of court this 29th day of November, 2023

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAJI**

## TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA WAMI/ RUVU

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Wami/ Ruvu. Bodi hii iliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 22 ambapo muda wa Bodi ni miaka mitatu.

**MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA WAMI/ RUVU**

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa:

**Katibu Mkuu,**
**Wizara ya Maji,**
**Mji wa Serikali,**
**Mtaa wa Maji,**
**S.L.P. 456,**
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: **ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika **"Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Wami/ Ruvu"** nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya **Jumatano tarehe 21 Februari, 2024 saa 09.30 alasiri**

**Imetolewana:**

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**
**11 Januari, 2024**

# Ndege ya mizigo ATCL sasa kutua Guangzhou

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Ndege ya (ATCL), imesema kutokana na mahitaji makubwa ya usafirishaji wa shehena kati ya China na Tanzania, ndege yake ya mizigo ya Boeing 767-300F inatarajia kuanza safari za China kuanzia mwishoni mwa mwezi huu.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Ladislaus Matindi, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wafanyabiashara kutoka Jimbo la Jiangsu la nchini China wakati wa sherehe yao ya kuukaribisha mwaka mpya.

Alisema wako katika hatua za mwisho za kupata kibali cha ndege yao kuanza safari nchini humo na kuahidi kwamba ndani ya muda mfupi wataanza kuchukua mizigo kutoka China na kutoka Tanzania kupeleka nchini humo.

"Mahitaji ya kusafirisha mizigo ni makubwa na kwa sasa tumekuwa tukisafirisha mizigo kwa ndege yetu ya abiria kwa wastani wa tani kumi hadi 15, lakini tukianza kutumia ndege ya mizigo tutavutia wafanyabiashara wengi zaidi kutumia ndege yetu," alisema.

Alisema ATCL imewapa unafuu wafanyabiashara wa China wanaotaka kutumia usafiri huo na watakaokuwa kumi kwa mkupuo mmoja watapunguziwa nauli ya kwenda na kurudi.

Aliwahamasisha wafanyabiashara hao kutumia usafiri wa ndege hizo kwa kuwa ni wa moja kwa moja tofauti na ndege za mashirika mengine ambayo hulazimika kutua kwenye vituo zaidi ya viwili kabla ya kufika nchini China.

"Sisi ndege yetu ikitoka hapa ni moja kwa moja China, ni wastani wa saa 11 kwasababu hatuna kituo tukisharuka Dar es Salaam ni mpaka China kwa hiyo wafanyabiashara mtaokoa muda wa kukaa kwenye nchi mbalimbali na kama mnavyojua muda ni mali," alisema Matindi.

Kwenye tukio hilo, Matindi alichezesha droo na wafanyabiashara saba kutoka kwenye jumuiya hiyo walipata tiketi za kwenda na kurudi nchini China kwa kutumia ndege ya kampuni hiyo. Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa China nchini, Tony Lu Zhang, alisema idadi ya raia wa China wanaokuja Tanzania kuwekeza imeongezeka maradufu kutokana na mazingira mazuri ya biashara yaliyowekwa na serikali.

Alisema hata kiwango cha shehena kinachofika kwenye Bandari ya Dar es Salaam kimeongezeka maradufu hali inayoonyesha mazingira ya uwekezaji yanazidi kuwavutia watu wengi zaidi.

"Ukienda bandarini utakuta meli zimepanga foleni kwaajili ya kushusha shehena sasa ukiona hivyo usidhani kwamba Mamlaka ya Bandari hawafanyi kazi vizuri bali ni kwasababu meli zimekuwa nyingi sana kuliko kawaida kwa hiyo zinalazimika kusubiri muda mrefu kupakua mzigo," alisema Zhang.

"Uchumi unaendelea kukua na biashara nayo inaendelea kushamiri zamani ukiagiza mzigo ulikuwa unafika baada ya siku 30, lakini sasa hivi zinaweza kufika siku 40 kwasababu watu wanaoagiza mizigo ni wengi sana huu ndio ushahidi kwamba biashara inaendelea kukua sana," alisema.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Murilo, alisema Jeshi la Polisi limejitahidi kuweka mazingira ya usalama ili kuwawezesha wafanyabiashara kufanya shughuli zao kwa utulivu.

Alisema zamani ilikuwa kawaida kwa wafanyabiashara hasa wa kutoka China kuvamiwa na kuporwa bidhaa na fedha, lakini Jeshi la Polisi limejitahidi kukabiliana na wahalifu na tayari imekomesha vitendo hivyo kwa kiasi kikubwa.

"Kwa muda mrefu tumekuwa tukishirikiana na jumuiya zenu kwa mambo mengi na nadhani mnakumbuka hali ilivyokuwa wakati ule wafanyabiashara wenzenu wanavamiwa, lakini tuliapa kwamba tutavitokomeza kwa sasa matukio kama hayo huwezi kuyasikia tena," alisema Muliro.

Alisema Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha ulinzi na usalama mkoani Dar es Salaam kuhakikisha wafanyabiashara wanafanya shughuli zao kwa amani na bila woga wa kuvamiwa.

# TRA kutatua ucheleweshaji mizigo katika Bandari ya Dar

**Na Halfani Chusi**

KAMISHNA Mkuu Mamlaka ya Mapato (TRA), Alphayo Kidata, amesema katika kupunguza adha ya mizigo ya wafanyabiashara kukaa muda mrefu bandarini, sasa imeweka mfumo wa uondoshaji wa shehena au bidhaa katika bandari unaowawezesha mfanyabiashara kufanya kila kitu mtandaoni mpaka mzigo unafika anakuwa tayari amefuata taratibu zote na kuupata kwa haraka.

Kidata aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam pembezoni mwa mkutano wa 51 wa Makamishina Wakuu wa Mamalaka za Mapato Jumuiya ya Afrika Mashariki ulioanza jana na unafikia tamati leo.

Alisema kwa sasa wako katika majadiliano ya kuangalia namna ya kuondoa adha hiyo, ili wafanyabiashara wapate mizigo kwa wakati na kulipa kodi.

Kuhusu mkutano huo, Kidata alisema lengo kubwa ni kuzungumzia sera za kodi na sheria zinazokinzana katika ukanda wa Afrika Mashariki na kuzitafutia ufumbuzi, kuongeza ushirikiano wa kikanda ili kuboresha makusanyo kwa maendeleo endelevu na kuwa mamlaka jumuishi katika usimamizi wa mapato.

"Mkutano huu huwa unafanyika mara mbili kila mwaka. Lengo kuu ni kuwa na soko la pamoja, tunafanya biashara kwa pamoja, tunafahamiana kwa mengi. Kunapokuwa na sera haiko sawa, tunazungumza, tunaiweka sawa.

Alisema mbali na maeneo hayo, pia kuna eneo la magendo ambalo linaathiri nchi. Mkutano huo utasaidia kupeana taarifa na kufanya oparesheni kwa pamoja kama Jumuiya ya Nchi za Afrika pamoja na kuangalia sera ya kodi inayoathiri upatikanaji kodi kwa nchi nyingine.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa nchi za Afrika Mashariki, Kamishna Mkuu wa Kodi Mamlaka ya Mapato Uganda, John Musinguzi, alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa umebeba mambo aliyoyaita nyeti kuhusu masaula ya kodi.

Awali akifungua mkutano huo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha nchini, Dk. Natu Mwamba alisema mkutano huo ni muhimu kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa umekutanisha makamishna wakuu wa kodi. Yatakayojadiliwa yataleta tija katika ukusanyaji kodi.

Nchi zinazoshiriki mkutano huo ni mwenyeji Tanzania, Uganda, Kenya, Sudani Kusini, Rwanda na Burundi.

TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

# MAOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA YA MSAADA WA KIUFUNDI NCHINI TANZANIA: KUMBUKUMBU NA. 0000000455

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA**
Kama sehemu ya dhamira ya kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd ya kukuza watoa huduma wa ndani na ushiriki wa Watanzania katika mnyororo wa thamani wa Mafuta na Gesi, hivyo, EACOP inatafuta mtoa huduma wa nje ya kampuni atakayesaidia kutoa huduma ya ajira na usimamizi wa ujuzi unaotakiwa katika Mradi.

Huduma zitakazotolewa ni kwa uchache ni pamoja na:
Mchakato wa Kuajiri: Utafutaji wa watahiniwa na ukaguzi wa vigezo.
- Kufanya ukaguzi wa watahiniwa wanaoendana na maelezo ya kazi yaliyotolewa na mradi.
- Kufanya tathmini za watahiniwa kwa njia ya usaili na uchuchaji.
- Kuhakiki sifa za kitaaluma za watahiniwa.
- Kufanya ukaguzi wa historia ya watahiniwa /marejeleo ya tabia au sifa zao.

Mara baada ya kuchaguliwa, Mtoa Huduma atawajibika katika usimamizi na utoaji Msaada wa Kiufundi kwa Wafanyakazi wote, ikiwa ni pamoja na:
- Kusimamia usaili na watoa huduma wapya katika mradi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanafuata sheria na miongozo ya ushiriki.
- Kuwajibika katika mahitaji yao yote ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi za afya kuhusu utimamu wa mwili kufanya kazi, upatikanaji, vibali, na kutoa nyaraka muhimu kwa watoa huduma wapya katika mradi.
- Kusimamia na kutoa Mikataba kwa watoa huduma wapya, kusimamia utendaji, zamu za kazi, likizo, hatua za kinidhamu, kusimamishwa na kuondolewa kwa watoa huduma wapya katika mradi.
- Kuwajibika katika gharama za Watoa Huduma, ikiwa ni pamoja na malipo, usafiri, malazi na gharama za matibabu.

Wakati akitekeleza majukumu yake, mtoa huduma wa nje atalazimika:
- Kuonyesha utaalamu wa hali ya juu na kuwa mwangalifu kwa kutumia maarifa, na umahiri katika utoaji wa huduma ili kuuwezesha Mradi.
- Kuzingatia sheria zote husika za kazi za nchi, sheria nyingine muhimu za nchi, sera na kanuni za EACOP na viwango bora vya utendaji wa kimataifa katika sekta ya mafuta na gesi ikiwa ni pamoja na viwango vya haki za binadamu na ubaguzi (ubaguzi wa kijinsia, asili au kikabila).
- Kuwa na uwezo wa kubadilisha mfanyakazi/mkandarasi yeyote ndani ya Mradi asiyeweza kutoa huduma.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au taasisi zinzoonesha nia zanaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Cheti cha Usajili na Ukaguzi wa hivi karibuni kutoka BRELA (ambatanisha nakala)
- Uthibitisho wa usajili wa mamlaka husika ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), n.k
- Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka uliopita (ambatanisha nakala)
- Uthibitisho wa leseni ya Biashara
- Uthibitisho wa uzoefu wa kutoa huduma zinazofanana na hii katika miradi au kampuni ikiwa ni pamoja na barua za uthibitisho kutoka kwa wateja wa hivi karibuni.
- Wasifu wa wafanyakazi muhimu watakaohusika katika mradi, ikiwa ni pamoja na viwango vyao vya elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma zinazohitajika.
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia,
- Kuzingatia Kanuni za Watoa Huduma wa Ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa Makampuni ya Ndani
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Haki za Binandamu

Kampuni yenye nia, ambayo ina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma ilizotajwa hapo juu inapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00 jioni** kwa saa za Afrika Mashariki (EAT) mnamo au kabla ya tarehe **21/02/2024**. Kichwa cha Barua pepe kiwe **HUDUMA ZA MSAADA WA KIUFUNDI EOI- 0000000455** (Kumbukumbu namba ya EOI iliyotajwa hapo juu). Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20. Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza.

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia ili kutoa orodha ya makampuni ya awali yenye vigezo. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji waTaarifa (NDA).

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

# MOMBI YA KUONESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA UANDAJI WA MICHORO, USANIFU WA PICHA NA VIELELEZO. KUMBUKUMBU NA. 00000343

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (''EACOP LTD''), inaalika kampuni yenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa Huduma ya uandaji wa mchoro, usanifu wa picha na vielelezo kwa ajili ya mradi wa EACOP.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi Kwenda katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani karibu na Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 296 zitakuwa nchini Uganda na kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA YA HUDUMA:**
Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) linatafuta mtoa huduma mwenye vigezo kutoa huduma ya uandaji wa mchoro, usanifu wa picha na vielelezo kwa ajili ya mradi wa EACOP. EACOP inaendesha shughuli zake katika mikoa minane (8) ya Tanga, Manyara, Dodoma, Singida, Tabora Shinyanga, Geita na Kagera ambako bomba limekatisha na vituo vingine vya uendeshaji bomba vimejengwa.

Mtoa huduma anatarajiwa kutoa huduma zifuatazo:
- Kusanifu na kuandaa vifaa mbalimbali vya mawasiliano, kwa uchache, ikiwa ni pamoja na, majarida, vipeperushi, mabango, mabango ya vitambaa , mitandao ya kijamii na michoro ya tovuti.
- Kuandaa wazo na kusanifu miundo mbalimbali ya mawasiliano ya kidijitali ya ndani na nje.
- Kukuhakikisha usanifu unaovutia , na unaofaa kulingana na miongozo ya chapa za jumbe za EACOP.
- Kundaa modeli ya usanifu na miongozo wa mitindo kwa ajili ya uandaji wa zana za mawasiliano zinazofaa.
- Kuwezesha ushirikiano na timu ya mawasiliano ili kuhakikisha kwamba miundo ya usanifu inawiana na malengo na dhamira ya ya kampuni.
- Kushirikiana na watoa huduma wengine , ikiwa ni pamoja na wachapishaji, ili kuhakikisha kuwa vifaa vyote vinatengenezwa kwa viwango vya juu zaidi.
- Anapaswa Kuhudhuria mikutano kama inavyohitajika ili kujadili maendeleo ya mradi na kutoa mrejesho wa usanifu.
- Kuwa na mchakato madhubuti wa kudhibiti ubora ili kuhakikisha michoro na usanifu inakidhi viwango na sifa za EACOP.

**MINIMUM REQUIREMENTS:**
Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinakaribishwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa uwezo wa kiufundi kama vile vifaa, miundombinu, na muundo wa timu
- Uzoefu uliothibitishwa wa kufanya kazi katika miradi mikubwa yenye mahitaji makubwa huduma inayoolewa
- Cheti cha usajili wa Kampuni na lesini ya biashazr vyote vinavyotolewa na BRELA
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Mlipa Kodi kwa mwaka uliopita
- Waombaji wanasisitizwa sana kuhakikisha kuwa wamesajiliwa kwenye kanzidata ya EWURA (LSSP) ya Watoa Huduma za Ugavi wa Ndani, wakati wa kuwasilisha maombi ya kuonesha nia.
- Kukidhi Kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na fasili ya Kampuni ya Ndani
- Uzoefu, utendaji na uwezo katika kutoaHuduma kama hizo zilizoainishwa hapo juu nchini Tanzania, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Uthibitisho wa wasifu wa wafanyakazi mhimu watakaohusika katika kutoa huduma za mradi ikijumuisha vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma husika.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa za fedha ya miaka mitatu iliyopita.
- Ushahidi wa sera na Mifumo ya Usimamizi wa shirika la HSE, utaratibu na mchakato kwa mujibu wa viwango vinavyotumika vya ndani na Viwanda kwa kazi zinazofanana.
- Uthibitisho wa kupiga vita rushwa, ufisadi, kwa kuzingatia Haki za Binandamu.

Makampuni yenye nia, uwezo na rasilimali za kutosha kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu zinakaribishwa kutuma maombi pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **procurement.tz@eacop.com**, (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb). Maombi yatumwe kabla au mnamo tarehe **06 Februari 2024** saa 11 jioni saa za Afrika Mashariki. Kichwa cha Barua pepe kiwe **REQ-00000343- kutoa uandaji wa mchoro, usanifu wa picha na vielelezo Mradi wa EACOP**. Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20 Maombi yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiingereza

**Muhimu:** Kampuni ya EACOP LTD itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia kulingana na EOI hii na kisha kufanya tathmini kwa kutumia vigezo vya ndani ili kubaini makampuni yatakayojumuishwa kwenye orodha ya (Makampuni) ya awali yaliyokidhi vigezo. Makampuni yaliyofuzu hatua za awali pekee ndiyo yatakayopewa mwaliko wa zabuni, kwa kutia saini Mkataba wa Kutunza Siri (NDA), kama mwendelezo wa wito wa mchakato wa utoaji wa zabuni. Kampuni ya EACOP LTD inayo haki ya kufanya maamuzi yake ya kuchagua au kukataa kampuni na kuheshimu maamuzi yake pasipo kutoa sababu kwa kampuni husika.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Agizo la Waziri Ummy litekelezwe kwa vitendo

**HIVI** karibuni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alitoa tamko kwa hospitali zote za serikali zinazozuia miili ya marehemu kuchukuliwa na ndugu zao kwa sababu ya kukosa pesa za kuikomboa.

Agizo hilo la Waziri Ummy linatokana na usumbufu wanaokumbana nao ndugu wa marehemu wanapotaka kuchukua miili ya ndugu zao kwa ajili ya kwenda kuipumzisha kwenye makao yao ya milele.

Tatizo hilo huwakumba ndugu wengi kutokana na kutomudu gharama za kulipia za kuichukua miili hiyo kwa kuwa wanatoka kwenye uuguzaji ambako hutakiwa kulipia huduma na hatimaye ndugu yao anapofariki wanakuwa hawana pesa hizo.

Wananchi wengi wanaishi katika hali ya kipato cha chini na inapotokea ndugu kupata maradhi, humuuguza kwa kuchangishana tena michango yenyewe hupatikana kwa taabu.

Agizo la Waziri Ummy limekuja baada ya ziara ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Paul Makonda, kumtaka atolee ufafanuzi wa baadhi ya wananchi kuzuiwa maiti hospitali kutokana na kudaiwa.

Tatizo hilo limekuwa likiwakera Watanzania wengi kwa hospitali kuzuia miili baada ya ndugu kushindwa kulipa gharama alizokuwa akitibiwa mpendwa wao.

Katika ufafanuzi wake Waziri Ummy ameeleza kuwa hospitali zote za serikali ni marufuku kuzuia maiti ya Mtanzania yeyote.

Maelekezo hayo ni ya serikali na yeye akiwa waziri mwenye dhamana amesisitiza hasa kwa kuzingatia misingi ya dini ambayo mtu akifariki anatakiwa kuzikwa siku hiyo hiyo.

Waganga wafadhili wa hospitali zote za serikali wametakiwa kuzingatia miongozo ya kutozuia maiti watafute njia nyingine ya kuruhusu ili ndugu waende kuzika watakapomaliza wataenda kudaiana mambo mengine.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Makonda ambaye alifarijika na majibu hayo aliweza umuhimu wa wananchi kupatiwa huduma muhimu kwa kuwa bila wao hakuna kiongozi anayeweza kuwa madarakani kwa sababu wanachaguliwa kupitia vyama na wapiga kura ni wao.

Wananchi hao wakati mwingine hulazimika kuuza mali zao ili kuwatibu ndugu zao na agizo hilo likitekelezwa litaleta faraja kwa wananchi.

"Kwa kuwa mimi ni msemaji nitahakikisha hakuna mwananchi atakayeteseka ukishafiwa kwanza ni pigo wengine wanafiwa na baba zao, mama ama mtoto hawezi kuwapata tena tunaishukuru serikali,"

Waziri Ummy alionya kuwa baadhi ya watumishi wa afya kutozingatia maelekezo ya maadili na miongozo mbalimbali katika kutoa huduma za afya.

Kauli yake ni kwa watumishi wa afya wanaokwenda kinyume na miongozo na maelekezo ya serikali kuchukuliwa hatua mara moja na viongozi wa mikoa na wilaya pale watakapobainika kufanya uzembe.

Alikiri afya ni jambo kubwa na ni gumu, linabadilika na wanaendelea kuongeza msuli kusimamia sekta ya afya kwa kuitaka mikoa na wilaya kuwajibika kwa mambo yote yanayotokea katika mikoa yao na wilaya zao.

Watumishi wa afya wa hospitali ambao hawana lugha nzuri wanapotoa huduma kwa wajawazito na wengine wakiwa bize kwenye simu badala ya kuhudumia wananchi wanatakiwa kuchukuliwa hatua mara moja.

Hata hivyo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Japhet Simeo, alisema tayari jambo hilo limelifanyiwa kazi.

Kwa hili agizo la Waziri Ummy, tuna imani sasa hakutakuwa na malalamiko ya wananchi kuzuiliwa miili ya ndugu zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Tuache kuyachafua mazingira tunajiua

**MVUA** zinazoendelea kunyesha zinaongeza hofu hasa kutokana na tatizo kuathiri miundombinu ya asili na muhimu ya kusafirisha maji kuyapeleka baharini.

Ukiangalia uotoasilia kama misitu, nyasi na vichaka ndivyo vinavyosaidia maji ya mvua kuingia ardhini taratibu na hatimaye kufikia sehemu za chini ambako kuna mifumo ya asili ya mifereji ya kuyasafirisha maji chini ya ardhi hadi kufikia sehemu za chemichemi, vijito, mito na mikondo.

Miundombinu mingine asilia ni mito inayopeleka maji kwenye maziwa na baharini, mathalani kwa Tanzania ipo mingi ni kama kila mkoa una mto mfano Dar es Salaam kuna Msimbazi, Pwani uko Rufiji na Wami wakati Morogoro kuna Ruaha-Mkuu na Kihansi kadhalika mkoa wa Ruvuma kuna mto Ruvuma.

Kwa upande wa maziwa mkoani Kagera na Mara kuna mito inayopeleka maji Ziwa Victoria aidha, Kigoma na Katavi na Rukwa kuna mingine mingi inayofikisha maji Ziwa Tanganyika.

Zama hizi uharibifu mkubwa wa mazingira asilia unahatarisha maisha ya watu mathalani, mafuriko ya mara kwa mara kama yanayotikisa Dar es Salaam kuanzia Ijumaa .

Ni ukweli, mabadiliko tabianchi yapo na yanaendelea lakini yote hayo ni matokeo athari hasi kutokana na fikra, sera na maamuzi ya mataifa na binadamu sehemu mbalimbali duniani hadi kiasi cha kuhatarisha mazingira kama inavyotokea.

Mabadiliko tabianchi kimsingi chanzo chake kikubwa ni ongezeko la joto duniani, kutokana na viwanda kuzalisha bidhaa mbalimbali na kuongeza moshi unaokwenda juu angani,

Aidha, pia matumizi ya nishati zinazochafua anga kama visukuku hasa mafuta, makaa ya mawe, gesi, kuni na mkaa unaotoa hewa chafu zote zikiingia kwenye anga la juu.

Kwa kiasi kikubwa vyanzo hivyo siyo rafiki kwa mazingira kutokana na kuzalisha gesi ukaa kwa wingi ambayo ni sababu kubwa ya kuongeza joto duniani hivyo kuchochea mabadiliko ya tabianchi yanayoleta mvua nyingi, upepo mkali, ukame, vimbunga na baridi kali kwenye maeneo mengine.

Uzalishaji wa hewa ukaa ni mkubwa na umeharibu ukanda wa ozoni inayoruhusu mionzi ya jua kupenya kirahisi hadi kwenye ardhi na kusababisha joto kupanda. Tanzania na bara la Afrika wanazalisha gesi ukaa kwa viwango vya chini lakini shughuli za viwanda huko Ulaya, Marekani, China na mataifa yaliyoendelea yanazidi kuchafua dunia, hivyo hakuna anayenusurika.

Lakini, siyo suala la kujitetea kuwa taifa halichangii hewa ukaa angani lina mchango kama kufyeka misitu na mapori na kuichoma moto hovyo.

Kadhalika kilimo na ufugaji usio rafiki kwa mazingira; wakulima na wafugaji hufyeka misitu, mapori, mbuga bila kujali huku wakiingiza makundi ya wanyama kwenye mito na maziwa bila kujali kila wanapoambiwa kuwa wanaathiri mazingira.

Kwa wafugaji huchoma moto kupata nyasi kulisha mifugo yao au kufukuza wanyama wakali nako ni kuharibu mazingira.

Kwenye nyumba kila siku watu hutumia kuni na mkaa na kuharibu misitu lakini pia kuongeza joto angani.

Ni wakati wa kujua kuwa kama hakuna kutunza mazingira mateso na athari za mvua kuanzia mafuriko yanayoua watu, kuharibu miundombinu, mazao, makazi na kuvuruga maisha havitakoma.

Ifike kipindi Watanzania wajue kuwa mvua zikiendelea njaa itazidi maana mazao yanaharibika. Barabara na madaraja vitabomoka, nyumba nazo zitavunjika, watu kufa na mifugo pia.

Hivyo juhudi za kutunza mazingira zianze sasa watu wapande miti, wasiharibu misitu, mapori na kuacha kutegemea zaidi mkaa. Serikali isimamie maelekezo yake kwa wananchi kulinda mazingira mfano ifuatilie ulinzi wa mito, misitu na mabonde yasiharibiwe na wafugaji, wakulima na waharibifu wa misitu.

Aidha, izingatie uwekezaji kwenye nishati ili ipatikane kwa gharama nafuu na kupunguza kutumia kuni na mkaa unaomaliza misitu.

Si hivyo isimamie kazi za kupanda miti ya asilia kuanzia vijijini na mijini pamoja na kuondoa wananchi kwenye maeneo hatarishi mfano mabondeni, milimani na kwenye sehemu za kimkakati zenye hifadhi za maji.

Uharibifu wa mazingira ya pwani usikaliwe kimya miti ya mikoko, minazi na majani yanayolinda ardhi ya ufukweni kudhibiti mawimbi isimamiwe.

Ni kweli mabadiliko ya tabianchi ni janga la dunia lakini inawezekana kulikabili kama serikali itakuwa na utashi wa kisiasa kulikabili na kupunguza athari kwa Tanzania.

HABARI KITAIFA

# Othman: Ushabiki wa kisiasa ni sumu

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka wanachama wa chama hicho kujitenga na ushabiki wa kisiasa katika kuwapata viongozi.

Amesema wanachama wanapaswa kuendeleza hamasa ili kukijenga chama hicho na kutimiza dhamira ya kuwa taasisi imara nchini itakayochangia vyema maendeleo ya taifa.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alitoa rai hiyo jana alipozungumza katika mkutano mkuu wa uchaguzi wa Mkoa wa Dar es Salaam uliofanyika Kigogo.

Alisema ushabiki wa kisiasa ni sumu kubwa katika kuleta maendeleo ya chama na nchi kwa jumla, lakini hamasa husaidia katika kujenga na kuleta maendeleo kwenye chama na serikali kutimiza dhamira ya kusaidia maendeleo ya taifa.

Alisema Tanzania inaendelea kuwa maskini licha ya kuwa kitovu cha utajiri mkubwa na rasilimali za kutosha. Ni zao la sumu ya ushabiki wa kisiasa na viongozi wanashindwa kuwa na mbinu ya kutatua kero za wananchi na kuleta maendeleo.

Alisema siri kubwa ya maendeleo katika taifa lolote ni kuwapo uongozi thabiti wenye maono na marifa makubwa sambamba na moyo wa kujitoa na kujitolea kwa uaminifu katika kuitumikia nchi na wananchi wake kwa kutatua kero walizonazo na kuleta maendeleo.

Othman aliwaonya wananchi na hasa wanachama wa chama hicho kutomchagua mtu au kiongozi kwa kuzingatia ushabiki au kujuana kwa kuwa kufanya hivyo "ni sumu kwa maendeleo ya watanzania".

Alisema Tanzania imeshindwa kutumia rasilimali zake na kuwasaidia wananchi kiuchumi na kimaendeleo kutokana na viongozi wengi kuwa washabiki wakubwa wa kisiasa badala ya hamasa ya kujitoa na kujitolea kwa uadilifu katika kuleta maendeleo nchini.

Alisema ni jambo la aibu kwa nchi kama Tanzania hadi leo inaendelea kuagiza hata mafuta ya kula kutoka nje licha ya kuwapo rasilimali za kutosha zinazoweza kuzalisha bidhaa hiyo iwapo viongozi waliopo madarakani watakuwa na maono ya kutosha ya kuinua uchumi na maisha ya wananchi na kuleta maendeleo ya watanzania kwa jumla.

Alisema kuwapo kwa hali hiyo kunachangiwa na kuwapo viongozi wabovu wanaoshindwa kushughulikia kero mbalimbali za wananchi, jambo ambalo linahitaji nchi kufanya mabadiliko kwa watanzania kuchagua viongozi wenye uwezo na uchungu wa nchi yao katika kuleta maendeleo.

Othman pia alizungunzia migogoro kati ya wakulima na wafugaji, akisisitiza haipaswi kuwapo kwa kuwa Tanzania ina maeneo ya kutosha kwa ajili ya malisho ya mifugo na shughuli za kilimo.

Aliwaonya wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam kutochagua viongozi wanaoendeleza ubinafsi na fitna miongoni mwao. Ni jambo alilolitaja ni hatari si tu kwa mkoa huo bali pia taifa kwa jumla, hivyo kurudisha nyuma dhamira ya chama hicho.

Naibu Katibu Mkuu wa ACT-Tanzania Bara, Joran Bashange, akimkaribisha Othman, alisema watanzania wanahitaji mabadiliko kwa kuwa wamechoshwa na kila aina ya mikopo ikiwamo 'kaushadamu' na mingineyo ambayo imekuwa adhabu hata baadhi kufikia hatua ya kuzikimbia familia zao.

Othman amekamilisha ziara yake katika mikoa ya kusini mwa Tanzania. Alianzia wilayani Songea, mkoani Ruvuma kabla ya kuzuru Mtwara, Lindi, Pwani na kumalizia ziara hiyo jijini Dar es Salaam.

## 'Wasanii wawe mfano elimu ya huduma ndogo za fedha'

**Na Peter Haule,** MOROGORO

KAMISHNA Msaidizi Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha katika Wizara ya Fedha amewataka wasanii wanaoshiriki kutoa elimu ya fedha kwa wananchi kutoka Shirika la Kijamii linalojishughulisha na utoaji wa elimu ya uraia (TACCI), kuwa mfano kwa jamii kuzingatia sheria na kanuzi za uendeshaji wa shughuli za kutoa elimu ya huduma ndogo za fedha.

Janeth Hiza alitoa rai hiyo jana mkoani Morogoro wakati akifunga mafunzo ya elimu ya fedha kwa wasanii yaliyolenga kutoa elimu ya fedha kwa njia ya ubunifu wa sanaa.


"Wizara ya Fedha tunajipanga kwenda vijijini kutoa elimu ya fedha kwa kuwatumia wasanii wa ngoma, nyimbo na maigizo na tunatamani kuona wananchi wengi zaidi wanafikiwa kwa njia rahisi, lakini yenye ufanisi," alisema Hiza.

Aliwataka wasanii kuendelea kubuni sanaa zinazoelimisha jamii kwa kuwa kazi za sanaa zina mvuto na hazichoshi kuzisikiliza na kuzitazama, hivyo zikitumiwa kwa malengo chanya, zitatoa mchango mkubwa katika kusukuma gurudumu la maendeleo nchini.

Akizungumza kwa niaba ya wasanii wa TACCI, Mtaalamu wa Sanaa za Jukwaani, Harrison Kisaka, alisema elimu waliyoipata mwanzo ilikuwa na lengo la kuisaidia jamii, hasa vijijini.

Alisema elimu hiyo pia imekuwa msaada mkubwa kwa wajumbe wote wa mafunzo hayo, hivyo akaahidi kuwa watakuwa chachu ya uelewa na kutoa elimu hiyo kwa jamii inayowazunguka.

Alisema watatumia muda mrefu kuigiza, kuimba na kubuni sanaa ya ngoma zitakazojikita kwenye elimu ya fedha ili na wao watoe mchango wao kwa taifa.



Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, akikabidhi mfano wa hundi ya kiasi cha dola za kimarekani 10,000 kwa wawakilishi wa kikundi cha Tujikomboe cha mkoani Geita, Maria Mihayo (kushoto) na Chausi Kasura cha akina mama waponda kokoto zilizotolewa na taasisi ya NVeP inayofadhiliwa na Rais na Ofisa Mtendaji wa Kampuni ya Barrick ,Mark Bristow, katika hafla iliyofanyika katika Mgodi wa Bulyanhulu mkoani Shinyanga juzi. Kulia ni Rais na Mtendaji Mkuu wa Barrick, Mark Bristow, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MVUA KUBWA IKITIKISA

## Wizara yataka hatua kukabili athari kiafya

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Elimu ya Afya kwa Umma, Wizara ya Afya, Dk. Tumaini Haonga ametoa wito kwa wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za kiafya ikiwamo kudumisha usafi wa mazingira katika maeneo yao ili kuzuia magonjwa ya mlipuko.

Jijini Dodoma jana Dk. Haoga alisema mvua inaponyesha kuna uwezekano wa athari za afya zinazoweza kujitokeza ikiwamo uharibifu wa miundombinu ya majitaka, hali inayoweza kusababisha kusambaa kwa magonjwa ya mlipuko.

"Kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, kuna athari za kiafya zinazoweza kujitokeza ikiwamo uharibifu wa miundombinu ya majitaka ambayo yanaweza kuchangia au kuibua kusambaa kwa magonjwa ya mlipuko kama vile ugonjwa wa kipindupindu.

"Pia kuna uwezekano wa kuongezeka magonjwa yanayosababishwa na minyoo na homa ya matumbo. Kwahiyo, nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi wenzangu na jamii kwa ujumla kwa kipindi hiki mvua inaendelea katika maeneo mbalimbali, wazingatie kanuni za afya kwa kudumisha usafi wa mazingira na kuepusha maji kutuama kwenye maeneo ya makazi," alisema.

Ikumbukwe kuwa kutokana na utabiri wa hali ya hewa uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA), kuna uwezekano wa kuwapo mvua juu ya wastani na hata El-Nino hadi Januari mwaka huu hasa katika mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Kigoma, Morogoro, Pwani , Dar Es Salaam, Tanga, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Umeme wa Bwawa la Nyerere waanza kuingizwa Gridi ya Taifa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Nyumba, Nishati na Maendeleo ya Makazi wa Misri, Assem Elgazzar, wakigusia maendeleo ya Mradi wa Uzalishaji Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) ambao kwa sasa umefikia asilimia 95.83.

Mazungumzo hayo yalifanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Waziri wa Misri akiongozana na watendaji wakuu wa kampuni ya JV Elsewedy na Arab Contractors (wanaotekeleza mradi wa JNHPP).

Kwa upande wa Tanzania, viongozi waliohudhuria ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme (TANESCO), Gissima Nyamo-Hanga.

Dk. Biteko alieleza kuridhishwa kwake na kazi kubwa inayofanywa na makandarasi pamoja na TANESCO huku akieleza kufurahishwa kwake na taarifa iliyotolewa na Makamu wa Rais wa kampuni ya Elsewedy, Wael Hamdy ya kuwa majaribio ya mtambo Na. 9 katika mradi wa JNHPP yameleta mafanikio na kilowati 100 zimeanza kuingizwa Gridi ya Taifa.

"Kikao hiki kimejikita kuzungumzia masuala mbalimbali kuhusu mradi wa JNHPP. Mheshimiwa Waziri Elgazzar ametumwa na Rais wa Misri kwa ajili ya kuona maendeleo ya mradi huu.

"Jambo lilitofurahisha hapa ni majaribio ya mtambo Na. 9 yanaendelea na kwa hatua ya mwanzo ambayo wamejaribu kuzungusha mtambo kwa njia ya maji, wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa na wameingiza kilowati 100 kwenye Gridi ya Taifa," alisema Dk. Biteko.

Alisema mafanikio ya majaribio hayo yanaleta matumaini kwa kuwa ratiba ya kazi imeanza mapema zaidi ya iliyopangwa mwanzo kutokana na kazi nzuri ya makandarasi pamoja na TANESCO. Lengo ni kuzalisha megawati 235 kutoka mtambo Na. 9 ifikapo mwezi ujao na kuendelea na mitambo mingine ikiwamo Na. 8 na Na. 7.

Alisema mradi huo ni wa kipaumbele cha Rais Samia Suluhu Hassan ili watanzania wapate umeme wa uhakika kwa kuwa mradi huo ukimalizika utaingiza megawati 2,115 katika Gridi ya Taifa.

Alisema katika kikao hicho walizungumza pia kuhusu masuala fedha zilizotengwa kwa ajili ya huduma za kijamii zinazotokana na kuwapo mradi huo ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya mkataba.

Dk. Biteko pia aliwaomba watanzania wawe na subira wakati serikali ikitekeleza miradi mbalimbali itakayoongeza umeme nchini ukiwamo mradi huo wa JNHPP.

JNHPP ni wa kielelezo kwa Afrika kwa kuwa unaonesha nchi za Afrika zinaweza zenyewe kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.

Waziri wa Nyumba, Nishati na Maendeleo ya Makazi wa Misri, Elgazzar, alisema nia ya serikali yao tangu mwanzo ni kuona mradi huo unakamilika kwa ufanisi na kwa wakati, akipongeza makandarasi na TANESCO kwa hatua nzuri ya utekelezaji wa mradi huo.

Alisema serikali ya nchi hiyo itaendelea kuwapa ushirikiano makandarasi hao katika hatua zote za utekelezaji mradi na kueleza kuwa kukamilika kwa mradi huo kutatoa fursa kwa kampuni za nchi hizo kuendelea kuaminika kwenye utekelezaji miradi mingine ikiwamo ya umeme.




Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dk. Natu Mwamba, akifungua mkutano jijini Dar es Salaam jana wa makamishna wakuu wa Mamlaka za mapato Afrika Mashariki, uliondaliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), (wa pili kulia) ni Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Alphayo Kidata. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kamati ya Bunge yataka utafiti wenye uhalisia, uwekwe wazi

**Na Renatha Msungu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo imeelekeza utafiti unaofanywa nchini uwe halisi na wazi kwa manufaa ya watanzania.

Akizungumza wakati akifanya majumuisho baada ya kutembelea maeneo mbalimbali ya Tume ya Taifa Sayansi na Teknolojia (COSTECH) mwishoni mwa wiki, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mussa Sima alisema mbali na utafiti huo kuwa wazi, usemwe hadharani ili wananchi waujue.

Mbali na hilo alisema wanahitaji kuona fedha iliyotengwa na Serikali inatumika ipasavyo ikilinganishwa na tafiti zinazofanyika katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

"Utafiti unaofanyika ushuke mpaka vyuo vingine vya kati, badala ya kuishia vyuo vikuu pekee," aliagiza Sima.

Kiongozi huyo wa kamati ambaye pia ni Mbunge wa Singida Mjini, alisema kamati imetembelea COSTECH kwa lengo la kuona kazi inayofanywa kulinganishwa na fedha zinazotolewa na serikali ili kuwajulisha wananchi kuhusiana na maendeleo yanayofanywa na serikali.

Mjumbe wa Kamati hiyo ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalum, Dk. Thea Ntara, alisema kuwa kati ya maeneo yenye shida ni vifungashio, wazalishaji wadogo wengi hawana uwezo mkubwa wa kukidhi soko la vifungashio.

Kutokana na changamoto hiyo, Dk. Ntara aliitaka COSTECH isaidie SIDO kupata ubunifu wa vifungashio kwa wingi na vyenye ubora.

Alisema tatizo la vifungashio limekuwa changamoto kwa wajasiriamali, hivyo SIDO wanapaswa kuliangalia hilo.

Mjumbe mwingine wa kamati hiyo ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Kusini, Nashon Bidyanguze, aliguswa na mbolea ya popo, akisema ni nzuri kwa wakulima japo mkojo wake una athari.

Kwa kuzingatia hoja hiyo ya athari, mjumbe huyo wa kamati akataka utafiti unaofanywa katika eneo hilo ujikite pia katika kusaka njia ya kuitumia mbolea hiyo bila kusababisha madhara.

Alisema watafiti wanapaswa kujua namna ambavyo mkojo wa popo unapaswa kutumika kama mbolea na kuwapa elimu hiyo wakulima ili waitumie bila kuleta athari yoyote.

Akiwasilisha mada kwa wabunge hao, Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu alisema COSTECH inasimamia, kuendeleza na kuanzisha kumbi nyingin za ubunifu.

Alisema tume hiyo pia imeanzisha na kuendeleza taasisi za uhawilishaji teknolojia nchi nzima kwa kushirikiana na vyuo vikuu na taasisi za utafiti.

# Wananchi wataka Jeshi la Polisi likamate wauaji

**Na Ambrose Wantaigwa**

WANANCHI katika Mji wa Sirari, wilayani Tarime, mkoani Mara wamelitaka Jeshi la Polisi kuwasaka waliofanya mauaji ya wenyeviti wawili wa vitongoji katika Kata ya Sirari na kuwafikisha mahakamani.

Kwa miaka miwili mfululizo wenyeviti wawili, Alex Chacha wa Kitongoji cha Nyatiti na Magasi Michael wa Kitongoji cha Gwitanka wameuawa.

Chacha aliuawa kwa kuchinjwa wakati Gwitanka aliuawa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali maeneo mbalimbali mwilini.

Kwa nyakati tofauti mwishoni mwa wiki iliyopita mjini Sirari, baadhi ya wakazi walisema kuwa kwa sasa wanaishi kwa hofu kwa kuwa wamepoteza imani na jeshi hilo kutokana na viongozi hao wa vitongoji vya kuuawa kikatili.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya hivi karibuni, ilieleza kwamba mtuhumiwa mmoja ambaye alitajwa kwa jina moja la Sinda, alikuwa anashikiliwa kutokana na mauaji hayo.

"Kama kiongozi anaweza kuuawa kikatili kwa kuchinjwa hadharani, sembuse sisi wananchi wa kawaida.

"Tunaogopa hata kufanya shughuli za kutuingizia kipato, tunaomba Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwafikisha kwenye mikono ya sheria wote waliohusika," alisema Marwa Chacha.

Akizungumza katika mazishi ya mmoja wa viongozi hao, Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara alikemea kuongezeka matukio ya mauaji ya viongozi, akisema tabia hiyo itachelewesha wananchi kujiletea maendeleo kutokana na kukosekana usalama.

Alisema haikubaliki watuhumiwa wa mauaji hayo kubaki huru wakati waliopoteza maisha ni viongozi walitokana na wananchi. Ukimya unasababisha hofu miongoni mwa wananchi wapenda amani.

"Eneo hili la Mji wa Sirari ni eneo la mpaka na nchi jirani, hatuwezi kukubali vitendo vya mauaji na uvunjifu wa amani vitokee tena kwa viongozi kwa kuwa vinazuia wananchi wa kawaida kuendesha shughuli za kujipatia kipato," alisema Waitara

Pia alikemea baadhi ya wanasiasa wanaoshabikia matendo ya uvunjifu wa amani. Viongozi wote waliouawa wanatokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katibu wa CCM Kata ya Sirari, Mahson Haruni aliomba serikali kufikiria kuwapatia kiinua mgongo wenyeviti wa vijiji na mitaa ili kuwezesha familia zao na wategemezi wengine kujikimu pale wenza wao wanapoteza maisha.

"Tunaomba sasa serikali ifikirie kuwalipa posho au kufuta jasho viongozi wa vijiji na mitaa ili wanapofariki dunia wakitekeleza majukumu yao familia zao zisiteseke," alisema Haruni.



# Mlundikano wa taka jijini Arusha wamkera Katibu CCM

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA



KATIBU wa Chama Cha Mpinduzi (CCM), Wilaya ya Arusha, Timoth Sanga, amemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Juma Hamsini kuwaelekeza wazabuni wote waliopewa kazi ya kuzoa taka kutekeleza jukumu hilo kwa wakati pamoja na kuwapa vifaa vibarua.

Sanga aliagiza hayo jana alipokwenda kusikiliza kero za wananchi wa Kata ya Moshono na Murieti.

Akiwa katika maeneo hayo, alikutana na mlundikano wa taka na malalamiko mengi ya wananchi kuhusu taka kutozolewa kwa wakati pamoja na taka kuzagaa mtaani katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

"Mkurugenzi, CCM haturidhishwi na hali ya uzoaji wa taka katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Arusha, kuna taka nyingi mtaani zilizokaa muda mrefu lakini pia wazubuni hawapiti kwa wakati na hawatoi vifaa vya kubeba taka kwa vibarua wao. Hii ni hatari kwa afya za wananchi wetu kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali," alisema.

Akijibu maagizo hayo kwa njia ya simu, mkurugenzi huyo alisema ameyapokea maagizo hayo, huku akiahidi kuyafanyia kazi mara moja.

"Nitawaandikia barua wazubuni wote, kuwakumbusha kuzoa taka kwa wakati na kuwapa vifaa vibarua wanaofanya kazi ya kupakia takataka kama mikataba inavyoelekeza,"alisema.

Awali, mkazi wa Moshono, Rehema Mollel, ambaye ni mama Ntilie jirani na Kituo cha Afya cha Moshono, alisema wanauza chakula katika mazingira magumu, kutokana na taka nyingi kulundikwa kwa muda mrefu jirani na eneo lao la biashara, hali inayosababisha harufu mbaya na wateja kushindwa kula chakula.

"Kituo cha afya kimeanza kulaza wagonjwa na wanategemea kupata chakula kutoka kwetu, lakini kutokana na hali ya hizi taka wanahofia kununua chakula chetu, wasipate magonjwa ya mlipuko hali iliyotulazimu kupeleka malalamiko kwa mwenyekiti wa serikali ya mtaa amtafute mzabuni wa kuzoa taka,"alisema.

Mkazi wa Kata ya Murieti, Francis Paschal, alisema awali gari la taka lilikuwa linapita mara mbili kwa wiki, lakini sasa linapita mara moja baada ya wiki tatu.

# Halmashauri Babati yaandikisha 75% wanafunzi darasa la awali

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

HALMASHAURI ya Mji wa Babati mkoani Manyara, imesema imefanikiwa kuandikisha wanafunzi wa awali kwa asilimia 75 mpaka sasa, huku zikiwa zimesalia siku siku 10 dirisha hilo kufungwa.

Akizungumzia jana kususua kwa uandikishaji huo, Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri hiyo, Simon Mumbee katika mahojiano maalumu na Nipashe, alisema kwa mujibu wa maelekezo ya serikali mzazi au mlezi ambaye hatomwandikisha mwanaye darasa la awali atachukuliwa hatua za kisheria.

Kutokana na hali hiyo amewaomba wazazi na walezi kuendelea kujitokeza kuwaandikisha wanafunzi hao, kabla ya kufungwa kwa dirisha hilo Machi 31 mwaka huu.

Mumbee alisema halmashauri hiyo ilianza uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali Septemba mwaka jana na ilijiwekea lengo la kuandikisha wanafunzi 4,027 ila mpaka kufikia Januari 19, ambapo walikuwa wameandikisha asilimia 75 tu ya lengo.

Ofisa elimu huyo alisema kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023, mwanafunzi wa awali anatakiwa kuandikishwa awe na miaka mitano na anapaswa kusoma darasa hilo mwaka mmoja tu.

"Huko nyumbani wanafunzi wa elimu ya awali wanakuwa wanatumia lugha za asili, hivyo elimu ya awali inawasaidia kuchangamana na wanajifunza Lugha ya Kiswahili, kusalimia na kucheza,"alisema Mumbee.

Mshauri wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC), Davis Gisuka, alisema mwanafunzi wa awali anatakiwa kupitia nyanja za kukua kiakili, kihisia, kimwili na kukuza lugha.

Kwa mujibu wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya 2030, haki ya watoto wote ya kupata elimu siyo tu lengo la nne la ajenda 2030, bali imewekwa katika mkataba wa haki za mtoto na mikataba na matamko mengine ya kimataifa, ambayo yanahitaji elimu ya msingi iwe bure na lazima kwa watoto wote.




Naibu Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo na Mbunge wa jimbo la Muheza Hamisi Mwinjuma Kulia juzi akimkabidhi funguo ya gari jipya la kubebea wagonjwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza Erasto Mhina Kushoto mwenye kofia ya chepeo ambalo litatoa huduma kwa wananchi wa Tarafa ya Amani wilayani Muheza, Watatu Kulia diwani wa kata ya Zirai Tarafa ya Amani Salimu Sechambo. **PICHA. NA STEVEN WILLIAM**

# Bilioni 2.75/- kujenga jengo la utawala halmashauri Monduli

**Na Allan Isack,** MONDULI

SERIKALI imepeleka zaidi ya Sh. bilioni 2.75 katika Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la halmashauri hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Isack Joseph, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu ujenzi wa jengo hilo.

"Tunaishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutupatia fedha za ujenzi wa jengo hili ambalo tayari limekamilika na litakuwa na idara zote za halmashauri na watumishi wote wa halmashauri na idara zote ziko hapa kwenye jengo moja,"alisema.

Alisema awali wananchi walipokuwa wanakwenda kwa ajili ya kutafuta huduma walijikuta wakibabaika na kuanza kuulizia sehemu wanayotaka kwenda kwa kuwa idara zilikuwapo maeneo tofauti tofauti.

"Kwa sasa wananchi wamerahisishiwa kupata huduma sehemu moja ambayo inawekwa ofisi zote, hivyo tunamshukuru Rais Samia kwa kazi kubwa aliyofanya kwenye halmashauri yetu,"aliongeza mwenyekiti huyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Monduli, Happiness Laizer, alipongeza serikali kwa kutoa fedha hizo kwa ajili ya kujenga jengo hilo.


"Jengo hili limegharimu takribani Sh.bilioni 2.75 fedha zilitotolewa na serikali na jengo limekamilika kwa asilimia 98 na imebakia asilimia chache kuweka mifumo mbalimbali, lakini limeanza kutumika tangu Novemba mwaka jana,"alisema Mkurugenzi huyo. Alisema watumishi wamefurahia kufanya kazi katika mazingira mazuri na imesaidia kuongeza ufanisi wa kazi kwa watumishi kuwahi kazini na kuendelea na majukumu yao.

Katibu Muktasi katika halmashauri hiyo, Firiliana Munisi, alisema awali walikuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kwa kuwa jengo walilokuwa wanalitumia lilikuwa ndogo.

Alisema: "Baada ya serikali kutujengea jengo jipya kwa kweli ufanisi umekuwa mzuri kwa watumishi kwa kuwa huduma zimekuwa karibu na hakuna mizunguko ya huku na kule, pia imewarahisishia wananchi kuhudumiwa kwa urahisi".

Ofisa Utumishi Halmashauri ya Monduli, Petro Mnashihuya, alisema changamoto iliyokuwapo wakati wakitumia majengo ya zamani ni usalama kwa watumishi katika utengaji kazi kwa kuwa majengo hayo yalijengwa miaka mingi iliyopita.

Alisema: "Majengo hayo ya zamani yalikuwa yanahatarisha usalama wa watumishi kwa kuwa yalijengwa miaka mingi iliyopita na yalikuwa hayaendani na viwango vya usalama mahala pa kazi".



# Viongozi ushirika waagizwa kutatua kero za wakulima

**Na Mohab Dominick,**
KAHAMA

VIONGOZI na watumishi wa vyama vya ushirika nchini wametakiwa kuwatumikia wakulima ikiwa ni pamoja na kusikiliza mahitaji yao, ili waweze kufikia malengo pamoja na kuinua sekta ya kilimo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Kaimu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Nchini, Colins Nyakunga katika Mkutano wa 28 wa Chama kikuu cha Ushirika Wilayani Kahama (KACU) na kuwataka wanachama endapo wakiona kuna kiongozi anakwenda ndivyo sivyo kutoa taarifa za haraka katika ngazi husika. “Tunataka kushirikisha watu katika jambo lolote ambalo linakuwa likitokea katika ushirika na pia muwe na nyezo zingine za kujipatia kipato tofauti na katika ushirika ambapo unakuwa mkifanya kazi,” alisema Nyakunga.

Alisema sheria inasema endapo kuna kiongozi anaongoza kwa kufuata maslahi binafsi ni heri akaondolewa kwa manufaa ya umma, huku akiwataka kutoingiza mambo ya siasa katika ushirika.

Kadhalika alitaja kuwepo kwa baadhi ya viongozi ambao wanakuwa wakiingia katika ushirika kutafuta nafasi katika siasa hali ambayo kwa sasa inabidi kukemewa kwa kiasi kikubwa kwani watu hao hawafai katika kujenga ushirika kiuchumi hapa nchini.

Hata hivyo aliwaonya makatibu na mameneja katika pamba kutumia fedha zinazotolewa na kampuni ya ununuzi wa zao hilo kwa kazi zilivyopangwa na kuacha matumizi binafsi ambayo ni kinyume cha sheria.

Ofisa kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Kahama, Frank Masilamba aliwataka wajumbe wa bodi ya ushirika pamoja na AMCOS kuwa wazalendo katika utendaji kazi wao kwa kutoa taarifa sahihi za ukomo wa madeni katika maeneo yao.

Masilamba alisema kutokutoa taarifa sahihi za madeni kumekuwa chanzo kikubwa cha wakulima kukosa malipo yao kwa wakati kunakosababishwa na madeni makubwa yaliyopo katika taasisi za kifedha hasa benki ambayo yamekuwa yakiwakopesha mara nyingi.

Alisema madeni kwa wakulima yamekuwa makubwa na kusababisha kushindwa kuyalipa, ambapo mpaka sasa bado wanaendelea na uchunguzi kwa lengo la kujua ni vyama vipi ambavyo mapaka sasa vimekuwa vikilaza madeni yake.

Alisema: “Madeni yamekuwa makubwa kwa wakulima na wengi wao wameshindwa kuyalipa kwa wakati na taasisi yetu bado tunaendelea na uchunguzi wa kujua ni vyama vipi ambavyo vimekuwa vilaza madeni mara kwa mara.”



Mkuu wa Wilaya ya Butiama Moses Kaegele akizungumza na wakandarasi pamoja na uongozi wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia alipotembea na kukagua mradi wa ujenzi katika Kampasi Kuu ya chuo hicho kilichopo Butiama Mkoani Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Manahodha, wamiliki vyombo vya majini wapewa onyo

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

MANAHODHA pamoja na wamiliki wa vyombo vinavyofanya shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo majini wameonywa juu ya ukiukwaji wa taratibu na sheria za vyombo vyao, ikiwemo ufanyaji wa safari nyakati za usiku kinyume na matakwa ya leseni zao.

Onyo hiyo imetolewa juzi na Katibu Tawala wa Mkoa wa Geita, Mohamed Gombati wakati akifungua kikao cha wadau wa usimamizi na usalama, ulinzi wa mazingira na usafirishaji majini katika Ziwa Victoria kilicholenga kujadili udhibiti wa ajali za majini.

Alisema wale ambao leseni zao zinawaruhusu kufanya safari za usiku hawana budi kuzingatia sheria na taratibu wakati wa safari zao, kwani ziwa linatumiwa na watu mbalimbali wakiwemo wavuvi, hivyo umakini wao utasaidia kudhibiti ajali.

Kadhalika aliwataka wavuvi kuhakikisha wanavaa vifaa vya kuwasaidia kuokolewa pindi inapotokea boti kuzama majini ikiwa ni pamoja na viashiria mwanga, ili kuzisaidia meli kubwa zinazofanya safari usiku kuwaona haraka.

Ofisa Mfawidhi wa Shirika la Uwakala wa Usimamizi Meli (TASAC) Mkoa wa Geita, Godfrey Chegere alisema mkoani Geita kuna vyombo vidogo vya usafiri wa majini vilivyo sajiliwa zaidi ya 2,000 wakiwemo wavuvi na katika ukaguzi uliofanyika mwaka 2023 vyombo 20 vilifungiwa na kupigwa faini kwa kukiuka sheria.

“Hatutawafumbia macho manahodha na wamiliki wa vyombo vya majini watakaobainika wakifanya kazi bila kuwa na usajili pamoja na kutofuata sheria kwa mujibu wa leseni zao, leseni ya boti ndogo inaelekeza kufanya kazi ya kusafirisha abiria na mizigo wakati wa mchana pekee,” alisema Godfrey.

Mratibu wa kituo cha utafutaji na uokozi kanda ya ziwa kutoka Shirika la TASAC, Joseph Mkumbo alisema kwa mujibu wa ripoti na tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa kila mwaka watu 5,000 wanafariki maji katika Ziwa Victoria wakiwemo wavuvi.

Mkumbo alisema kuwa katika kuhakikisha wanadhibiti matukio ya ajali majini shirika hilo linatarajia kuanzisha vituo vidogo vya utafutaji na uokozi katika wilaya za Sengerema, Chato na Geita huku akieleza kuwa tangu kuanzishwa kwa kituo cha utafutaji na ukozi katika kanda ya ziwa matukio hayo yamepungua.

## Wajasiriamali 100 wapewa mafunzo utengenezaji bidhaa

**Na Shaban Njia** KAHAMA

WAJASIRIAMALI wanawake zaidi ya 100 mkoani Shinyanga wamepewa mafunzo ya kutengeneza bidhaa zenye ubora unaohitajika katika soko huru la ushindani Afrika.

Licha ya kupewa mafunzo hayo wametakiwa kuchangamkia fursa za mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri ili kujiongezea mtaji.

Akizungumza wakati wa mafunzo kuhusu kanuni, taratibu na sheria za kufanya biashara kwenye soko huru la Afrika, Mkurugenzi wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake (TWCC), Mwajuma Hamza alisema kila mwaka wamekuwa wakiwafikia wajasiriamali zaidi ya milioni moja ili kuwapatia ujuzi.

Hamza alisema wajasiriamali wengi wanashindwa kukua kibiashara na kubaki ni soko la ndani kutokana na kushindwa kuwa na bidhaa bora, kutosajili biashara zao pamoja na kukosa nembo ya ubora kutoka Shirika la Viwanda Tanzania (TBS).

“Soko huru la Afrika linazaidi ya ushindani wa wajasiriamali bilioni 1.2 kutoka nchi 55 na ili tuweze kushindana nao na kupata masoko huko lazima tuwe na bidhaa zilizokidhi vigezo kutoka katika mamlaka zetu nchini,”alisema Hamza.

Aidha alisema wiki mbili zilizopita walikutana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji ambaye alisema tayari wizara imeanzisha mfuko maalumu wa kudhamini wafanyabiashara ambao wanapata fursa ya kuuza kwenye masoko ya nje.

Alisema Waziri aliwataka kuunda wasifu wa biashara zao ambazo wataziwasilisha wizarani ili wapate msaada kupitia mfuko huo.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita akifungua mafunzo hayo aliwataka wajasiriamali hao kuchangamkia fursa za mikopo isiyokuwa na riba ya asilimia 10 iliyokuwa ikitolewa na halmashauri awali.

Alisema kwa sasa serikali imeweka utaratibu mzuri ili itolewe na taasisi za kifedha ambazo zitaainishwa hapo baadae.

Nipashe
TESA
Jumanne Januari 23 , 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**Utoro kidato cha1 ulivyomshtua RC, aagiza J3 wote waripoti vinginevyo...**



Ukurasa 13

Shule 'kali' Mgaza hatarini yabaki kisiwa, barabara kikwazo kuifikia



Ukurasa 14

Mabadiliko tabianchi hayakimbiwi, kusaidia waathirika hakukwepeki

ELIMU

NA WAANDISHI WETU

UKEKETAJI KINAMAMA

# Ya nini mila inayoleta msiba, ulemavu na maradhi kwa jamii yako, ikatae

MIKOA ya Mara, Manyara na Arusha ni baadhi ya maeneo ambayo matendo ya ukeketaji wasichana hufanywa kwa sababu au madai mbalimbali.

Wapo wanaosema wanawakeketa kuhakikisha usafi wa mwili hasa sehemu za siri, yapo madai ya kuhifadhi ubikira, wengine wanadai ni kumfanya mwanamke aolewe au aoleke.

Maelezo mengine yanayotolewa ni kupunguza hamu ya tendo la ndoa kwa wanawake japo pia ukeketaji unatajwa kuwa hufanyika kuwaingiza wasichana katika utu uzima na kuwaweka tayari kuolewa.

Kukeketa ni kukata au kuharibu sehemu za siri za mwanamke. Baadhi ya wanajamii wanakeketa kutimiza mila na desturi zao, wengine wanaamini dini inawataka wafanye hivyo na wapo wanaofuata mkumbo kwa maana hawana sababu maalumu ya kufanya vitendo hivyo.

Kwa ujumla, vitendo vya ukeketaji vinasababishwa zaidi na msukumo wa mila na desturi za makabila yanayohusika zikiwamo imani za baadhi ya wanajamii.

Kwa mujibu wa taarifa ya hali ya afya na viashiria vya malaria ya mwaka 2022, asilimia nane ya wanawake nchini wamefanyiwa vitendo vya ukeketaji.

Inaitaja mikoa ya Manyara, Arusha na Mara kuwa kinara kwa kuwa na asilimia zaidi ya 30 ya wanawake waliofanyiwa ukeketaji, ikimaanisha kuwa katika wanawake 100 wa mikoa hiyo 30 wamekeketwa, kadhalika katika wasichana 10 watatu wamefanyiwa mila hiyo.



Baadhi ya vifaa vya ukeketaji vinavyotumiwa kuwaadhibu wanawake. **PICHA: MTANDAO**

Jamii zinazoendeleza vitendo vya ukeketaji ni zile zilizotawaliwa na mfumo dume na mila gandamizi kwa wanawake, hasa zikiangalia masuala ya kujamiiana na kutaka kuwadhibiti wanawake.

Zama hizi ukeketaji hufanywa kwa watoto wa chini ya miaka mitano na hasa wachanga kabla ya kufikisha siku 28 za kuzaliwa.

Hata hivyo jamii haijakaa kimya, miaka ya karibuni kumekuwa na juhudi za kupambana na vitendo vya ukeketaji nchini zikihusisha kampeni za kutoa elimu ya madhara, ushirikishwaji wa viongozi wa mila na dini pia jamii kubwa katika kupambana na vitendo hivyo.

**MADHARA**

Tanzania kama ilivyo kwenye nchi nyingine zinazoendelea, imeshuhudia madhara yatokanayo na ukeketaji kwa wanawake, ambayo ni pamoja na kusababisha maumivu makali sana kwa wasichana au wanawake wakati na baada ya ukeketaji.

Vifo vya wasichana na wanawake kwa kuishiwa damu kutokana na kuvuja damu nyingi baada ya kukeketwa na kukosa msaada wa kitabibu.

Aidha, vipo vifo vya wajawazito wakati wa kujifungua kutokana na kuvuja damu nyingi kwenye kovu litokanalo na kukeketwa hasa wale wanaojifungua kwenye maeneo yasiyo na huduma za afya.

Yapo maambukizi ya magonjwa kama VVU na UKIMWI na maradhi yanayotokana na majimaji ya mwili mfano homa ya ini.

Madhara mengine ni kinamama kutofurahia tendo la ndoa na pia wanawake kuathirika kisaikolojia, aidha, ndoa nyingi kuvunjika kwa sababu ya mwanamke kupitia vitendo vya ukeketaji kipindi cha utoto au ujana wao pamoja na kuumizwa na msongo wa mawazo.

Kwa ujumla wananchi wanapoteza rasilimali na maisha kutokana na vitendo hivyo vya ukeketaji kwa wanawake katika jamii wanapoishi.

Madhara yote haya yanadhoofisha sana nguvu hasa pale mwanajamii anapopatwa na vifo hivyo kushindwa kuendelea na majukumu yake ya uzalishaji mali na kutunza familia yake.

Na zaidi matatizo yatokanayo na ukeketaji yameathiri na kurudisha nyuma maendeleo katika nyanja za uchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa.

Mfano, taifa linapopambana kupunguza vifo vya wajawazito na kuongeza shule ili kuinua elimu kwa wanawake, ukeketaji unarudisha nyuma juhudi zote hizi.

**UFUMBUZI**

Ni wazi kwamba vitendo vya ukeketaji vina madhara makubwa katika maisha na maendeleo ya mwanamke na jamii yake hivyo, ni muhimu kuhakikisha inakuwa makini katika kuzuia na kutoa taarifa za dalili za kutendeka kwa vitendo kama hivyo.

Taarifa zifike polisi, viongozi wa vijiji, serikali za mitaa na kwenye asasi za kiraia ili mamlaka zichukue hatua stahiki kwa wakati.

Baadhi ya hatua zinazotakiwa kuchukuliwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma na kueleza jamii madhara ya ukeketaji kwa wanawake na taifa kwa ujumla.

Wito wetu ni huu: Kila mwanajamii aanze kuchukua tahadhari dhidi ya vitendo vya ukeketaji ili kuwakinga wanawake hasa wasichana zaidi kwa sasa ni kuwakinga watoto wadogo chini ya miaka mitano.

Hii ni pamoja na kuhakikisha watoto na watu wazima wanatoa taarifa za kuwepo kwa dalili za kutokea kwa vitendo hivyo katika maeneo yao wanayoishi ili kuwezesha kuchukua hatua na kuzuia uharibifu.

Aidha, serikali iongeze juhudi katika kuwabana wazazi, walezi na wanajamii wote wanaoshiriki katika kuendeleza vitendo vya ukeketaji kwa wanawake hasa kupambana na mtindo mpya wa kuwakeketa watoto chini ya miaka mitano muda mwingine watoto wachanga mara tu baada ya kuzaliwa.

Kadhalika wataalamu wa afya kutoa elimu kwa jamii kuhusu tatizo hilo la ukeketaji, madhara yake na hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa mapema ili kupunguza na kumaliza kabisa ukeketaji kwa wanawake.

Kama kila mmoja katika

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA SABATO KASIKA, MUSOMA

# Utoro kidato cha 1 ulivyomshtua RC, aagiza J3 wote waripoti vinginevyo...

INAKWENDA wiki ya tatu tangu shule za msingi na sekondari kufunguliwa, hapo Januari 8, wanafunzi wa madarasa ya awali na kwanza pamoja na wengine wakianza sekondari.

Ni mwanzo wa muhula wa masomo kwa mwaka huu wa 2024, wanafunzi wa kuanzia elimu ya awali hadi vyuo vya kati na vikuu, wakiendelea na masomo katika maeneo mbalimbali nchini.

Wakati wakisoma na kutafuta maisha bora kupitia elimu, kuna baadhi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao tangu shule zifunguliwe, hawajaripoti katika shule walizopangiwa wala hakuna mzazi au mlezi anayezungumzia hatima yao.

Miongoni mwa wanafunzi hao ni wa shule mbalimbali za mkoa wa Mara na sasa serikali inatoa maagizo maalumu, ni kutoka kwa Said Mtanda anawaagiza viongozi mbalimbali kuwasaka na kuripoti shuleni wiki hii.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa Mtanda, wanafunzi 20, 572 wa kidato cha kwanza hawajaripoti kwenye shule walizopangiwa.

Anafafanua kuwa jumla ya waliochaguliwa ni 52, 784 ili kujiunga shule za sekondari mkoani humo, lakini hadi kufikia wiki iliyopita Januari 17 ni wanafunzi 32, 212, sawa na asilimia 61.03 ya wote waliochaguliwa ambao wameripoti shule.

Mkuu wa Mkoa anawaambia wanahabari mjini Musoma mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa kuzungumzia mwendelezo wa ufuatiliaji wa tathmini ya ukaguzi wa shughuli za elimu mkoani humo .

Ukaguzi ulioanza Januari 8, mwaka huu muhula wa masomo unapoanza, ndiyo unaogundua utoro huo.

"Wanafunzi 20, 572 hawajulikani walipo, wakuu wa wilaya, viongozi wa halmashauri, wakurugenzi wa halmashauri, maofisa elimu kata, watendaji wa kata na vijiji tumieni wiki hii kufuatilia tatizo liko wapi na watoto waripoti shule haraka," anaagiza Mtanda.



Mkuu wa Mkoa wa Mara Said Mtanda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Aidha, anawataka wazazi na walezi kutowaficha watoto, na kwamba watajaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria ingawa hakufafanua hatua hizo.

Mbali na hao wa sekondari, anasema

kuna watoto walioandikishwa kuanza elimu ya awali na la kwanza, baadhi yao hawajaripoti.

"Wazazi na walezi wahakikishe wanawapeleka shule watoto wao haraka iwezekanavyo kabla ya Machi 31 watoto vinginevyo tutawachukulia hatua za kisheria," anasema.

**UANDIKISHAJI**

Aidha, kuhusu uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kwa mwaka 2024, Mtanda anasema, mwaka jana hadi Januari 17 mwaka huu, mkoa uliandikisha watoto 67,061 ambao ni sawa na asilimia 90.3 ya matarajia ya kupokea wanafunzi 74,234 wa kuanza darasa hilo.

"Lakini pia kati ya wanafunzi wote walioandikishwa kwa ajili ya kuanza darasa la kwanza, wanafunzi 107 ni wenye mahitaji maalum na tayari wameanza masomo yao " anasema.

Anafafanua kuwa wanafunzi 65,076 wameandikishwa darasa la awali wavulana wakiwa ni 32,499 na wasichana ni 32,577 sawa na asilimia 78.7 ya matarajio ya kuandikisha wanafunzi 82,679. na kwamba kati ya wote hao, 111 ni wenye mahitaji maalum.

"Katika uandikishaji huu, wanafunzi 503 wameandikishwa kwa ajili ya madarasa ya Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA), wavulana wakiwa ni 256 na wasichana ni 247," anasema.

**MUSOMA DC YAONGOZA**

Aidha, Mkuu wa Mkoa anaipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Musoma kwa kuongoza katika uandikiahaji wa wanafunzi wa madarasa ya awali, kwamba makadirio yao yalikuwa ni kuandikisha watoto 9,540, wameandikisha 9,318 ambao ni sawa na asilimia 97.57.

Akifafanua zaidi kuhusu uandikishaji huo Kaimu Katibu Tawala Msaidizi upande wa elimu wa mkoa huo, Makwasa Bulenga, anasema: "Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ilikadiria kuandikisha watoto 15,2400 lakini imeandikisha 9,852 ambao ni sawa na asilimia 65.57.

Anasema Wilaya ya Butiama imeandikisha watoto 9,287, wilaya ya Bunda watoto 7,188, Bunda Mji watoto 4,141 na Tarime Mji watoto 2,588 na wilaya ya Serengeti ilipanga kuandikisha watoto 12, 554, lakini imeandikisha 12, 134 ambao ni sawa na asilimia 96.65.

"Halmashauri ya Wilaya ya Musoma imeongeza kutokana na uhamasisha ji mzuri uliofanywa na watendaji kuanzia ngazi vijiji na wanaendelea hadi mwisho wa mwezi Februari," anasema Bulenga.

Bulenga anasema, anaamini kufikia wakati huo kila mtoto ambaye ameandikishwa kuanza shule atakuwa ameungana na wenzake kuendelea na masomo.

"Mkuu wa mkoa ametoa maelekezo kwa viongozi kuwafuatilia watoto wote ambao hawajaripoti shuleni wakiwamo wa sekondari, kinachofuata ni utekelezaji wa maagizo hayo," anasema.

## Ya nini mila inayoleta msiba, ulemavu na maradhi kwa jamii yako, ikatae

**INATOKA UK.11**

jamii atafanya hivyo taifa litakuwa na wanawake hasa watoto wenye afya na utimamu wa kimaumbile.

Ndivyo ilivyo kwa sasa kuhusu hali ya ukeketaji na madhara yake kwa wanawake kwani mara nyingi mila hizi hazisemwi sana katika jamii ila zipo na zinaleta madhara makubwa sana kwa wanawake.

Makala hii, inayoandikwa kuelekea wiki ya kupinga ukatili wa ukeketaji dhidi ya wanawake itakayoanza Februari 2 hadi 6 2024 hivyo kila mmoja akumbuke jukumu la kukomesha mila hii yenye kuleta maradhi, vifo, ulemavu na msongo wa mawazo.

**Waandishi Celina Paschal, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS). Pankras Luoga Mhadhiri Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya miradi ya MUHAS. Maoni: 0757-645746.**

ELIMU

NA IDDA MUSHI, MOROGORO

# Shule 'kali' Mgaza hatarini yabaki kisiwa, barabara kikwazo kuifikia





Wanafunzi wakihofia maisha kutokana na korongo linalozuia kufika shuleni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

LICHA ya jitihada za serikali kujenga shule mpya na za kisasa maeneo ya pembezoni, ambayo awali watoto walikosa elimu, ukosefu wa miundombinu timamu ni changamoto inayokwamisha kufikia elimu inayoboreshwa.

Mathalani Shule ya Msingi Mgaza iliyopo kata ya Mindu Manispaa ya Morogoro, ni furaha wanajamii kuwa na shule hiyo lakini pia ni kilio kwa kuwa inatishia uhai wa wanafunzi.

Ujio wa shule hiyo ya msingi bora na ya kisasa zaidi, umegeuka kitisho baada ya barabara wanayotumia watoto kwenda na kurudi shuleni kuharibiwa na kuwa na korongo kubwa linalotitia na lisilopitika.

Nyakati hizi za mvua pengine wananchi wangesema hali ni mbaya na hatari ni vyema kufunga shule.

Wakazi wa Mgaza na watumiaji wa barabara hiyo ambao licha ya kupongeza jitihada za serikali kutoa zaidi ya Sh.milioni 470 kujenga shule hiyo ya kisasa, miundo mbinu mibovu ya barabara inakwamisha wanafunzi hasa nyakati za mvua.

Aidha, maeneo mengine ya barabara hiyo yameharibika na kuwalazimisha wananchi kutoka Bondwa Madukani kutengeneza barabara nyingine mpya mbili za mashambani, ambazo nazo zimeharibika.

> "Shida ipo kwenye barabara ni mbovu, wanafunzi wanasoma vizuri lakini hatujui mvua inanyesha muda gani, wengine wanarudi nyumbani wamechafuka na tope kwa kuanguka. Tunaomba sana tusaidiwe kuokoa maisha,"anasema Neema Said.

Gaudance Mahwago, Calista Laston, Neema Said, Tunu Omary, Eric Fabian na Asha Abdul wakazi wa Mtaa wa Mgaza, kwa nyakati tofauti licha ya kupongezi serikali wana maombi maalumu ya kupata barabara.

Wanaomba barabara ili kwenda na usasa wa shule hiyo mpya ya msingi iliyoanza mwaka huu, sambamba na wanafunzi wa Sekondari ya Bondwa na watumiaji wengine.

"Ni juzi tu shule imefunguliwa, na viongozi wamepita hapa wakienda na kurudi kuikagua, na hata kuhakikisha wanafunzi wameanza masomo, sijui kama wameliona hili korongo, lakini linaonekana wazi, najua wameliona na karibuni ilikuwa inabeba boza la maji ilitumbukia korongoni," anasema

Rais Samia Suluhu Hassan, ametuwezesha kutupa shule nzuri lakini sasa tunahitaji Mkurugenzi wa Manispaa atusaidie ili wanafunzi waondokane na korongo na maji yanayobomoa barabara,"anasema Mahwago.

Tunu Omary anabainisha kuwa watoto wa chekechea na wa darasa la kwanza wa Mgaza kipindi cha mvua, hawaendi shuleni kwa hofu ya korongo hilo ambalo limeendelea kumega barabara kwa zaidi ya nusu na baadhi ya wananchi huhofia kuvuka.

"Shida ipo kwenye barabara ni mbovu, wanafunzi wanasoma vizuri lakini hatujui mvua inanyesha muda gani, wengine wanarudi nyumbani wamechafuka na tope kwa kuanguka. Tunaomba sana tusaidiwe kuokoa maisha,"anasema Neema Said.

Balozi wa shina namba nane mtaa wa Mgaza, Iddi Salum, anasema tatizo ni kubwa sio kwa eneo la Bondwa kwenye korongo lililokula barabara pekee, bali pia sehemu inayounganisha mtaa wa Mgaza na Lugala, ambako ni balozi wa mwisho mpakani kunakohitajika daraja.

Anasema mawasiliano ya barabara yamekatika kabisa na watumiaji wa njia hiyo wakiwamo wanafunzi hawawezi kuvuka upande mmoja kwenda mwingine.

Mwenyekiti wa mtaa wa Mgaza, Spencioza Modeli, anasema wanatambua changamoto hiyo kubwa ya barabara na hatari kwa usalama wa watoto, hasa wakati huu wa mvua, na wamepiga picha maeneo hayo na kuripoti ofisi ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini TARURA kwa hatua zaidi.

"Kama Mwenyekiti wa mtaa niliwahamasisha wananchi tukaweka viroba angalau tukaziba lakini mvua ni nyingi tumezidiwa nguvu, baada ya kuwapa picha na maombi TARURA wameahidi kuja, sijui lini, ila hali ya njia zetu sio rafiki ni mbaya mno,"Anasema Mwenyekiti.

Diwani wa kata ya Mindu ulipo mtaa wa Mgaza, Zuberi Mkalaboko, licha ya kumshukuru Rais Samia kwa kuwapatia zaidi ya milioni 470 kujenga shule hiyo mpya na ya kisasa na watoto kuanza masomo darasa la awali hadi la saba, changamoto hiyo kubwa ya barabara kwenda na kurudi shuleni anaitambua.

Anadai barabara hiyo iko chini ya TARURA na wamesharipoti na kwamba inazidi kuharibika zaidi kutokana na mvua zinazoendelea.

"Lakini juzi tukiwa kwenye kikao cha kamati ya wazazi pale shuleni baada ya masomo kuanza rasmi, tulikubaliana kuanza kuweka nguvu zetu ili watoto wapiti sehemu salama TARURA tumewapa taarifa ili washughulike,"Anasema Mkalaboko.

Meneja wa TARURA wilaya ya Morogoro Mohamed Muanda, anasema tatizo hilo linajulikana na barabara nyingine nyingi za manispaa ya Morogoro wanazosimamia ila kutokana na mvua zinazoendelea hali inazidi kuwa na changamoto zaidi.

"Kutokana na mvua barabara imekatika. Upya wa shule na uzuri wake unatulazimisha kujenga upya..."

Anasema kwenye ujenzi wa barabara wanaangalia mkandarasi aliyeko kazini kama alikuwa anajenga barabara ya changarawe kilometa moja, wanamwelekeza ajenge mita 800 na 200 zinazobakia anapelekwa kwingine kufanyakazi ya dharura.

Anaahidi kuwa kuna mkandarasi ukanda wa Mindu upande wa Lugala wameshapewa maelekezo ya kujenga barabara ya Mgaza na karibuni ataanza ukarabati barabara hiyo.

Anaongeza kuwa wanatambua jitihada za wananchi wa kata ya Mindu hususani mtaa wa Mgaza kusafisha maeneo ilipojengwa shule hiyo.

Muanda pia anawasihi wananchi wa katikati ya mji kuchukua tahadhari za kutunza mifereji ya kwani wakati inazibuliwa waache kutupa taka ovyo zinaziba makalavati na kubomoa miundombinu.

Anawakumbusha madhara ya maji hayo kuwa huingia kwenye makazi ya watu, kuumiza wananchi. kukata barabara hata madaraja na kusababisha maafa vikiwamo vifo na majeruhi.

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Mabadiliko tabianchi hayakimbiwi, kusaidia waathirika hakukwepeki



Mafuriko yanavyotishia maisha, mali na miundombinu.. **PICHA: MTANDAO**

MABADILIKO ya tabianchi hayakwepeki. Mvua kubwa, vimbunga baharini, mtetemeko ardhini na maporomoko ya milima kadhalika nayo hakuna namna ya kuyakimbia.

Mafuriko yametikisa nchi na wanaoathirika zaidi ni wale waliojenga karibu na mito, mabondeni na kwenye mikondo ya maji.

Mvua kubwa na mafuriko zimeumiza watu licha ya maonyo ya mamlaka ya hali ya hewa (TMA) na viongozi mbalimbali wa serikali kuhimiza kuchukua tahadhari na kusisitiza watu kuondoka maeneo hatarishi.

Licha ya kwamba hakuna maelezo ya idadi ya vifo lakini kuna ripoti za waliopoteza maisha na mali kutokana na mvua zilizonyesha mwishoni mwa wiki kuanzia Dar es Salaam, Pwani na Iringa.

Watu wanaofuatilia wanaona kuwa wanaoathiriwa hawapendi maisha yao au hawajipendi kwa sababu wameambiwa mara milioni nyingi wahame kwenye hatari. Inakuwaje hawapendi maisha yao?

Kupenda ni kutambua kitu kizuri na kuwa na hamu na ari ya kukimiliki. Hivi wapo ambao hata sasa hawajatambua kuwa maisha ni kitu muhimu,kizuri na cha kipekee na kila mmoja anatamani kukimiliki?

Jibu ni hapa, ni kama kila mmoja anatambua hilo na anayapenda maisha tena ikibidi aishi bila kikomo ila shida ni umaskini.

> Kituo cha Kimataifa cha Kupunguza na Kuokoa wanaopata Maafa (Global Facility for Disaster Reduction and Recovery) na Benki ya Dunia, zinasema madhara ya umaskini kwa watu wanaokumbwa na majanga yanakwenda mbali zaidi ya yale ya kiuchumi pekee.

Ni kweli kuwa jamii nyingi maskini ndizo waathirika au zilizo katika hatari zaidi ya kuumizwa na majanga hasa mafuriko kwa sababu ya athari kubwa za umaskini katika maisha yao ya kila siku.

Maeneo ambayo huathirika zaidi na mafuriko hasa mabondeni ndiko kwenye nyumba za bei nafuu zaidi, lakini pia watu wanaweza kufanya shughuli za ujasiriamali na uzalishaji kwa unafuu mfano kulima mboga na kufanya biashara nyingine bila kutumia gharama kubwa.

Mabondeni, milimani, ufukweni maziwani na kwenye mikondo ya maji ndiko kwenye hatari ya mafuriko wakati huu mvua zinapoendelea kunyesha usiku na mchana tena zisizotabirika.

Ikumbukwe umaskini ni tanzi. Una sura nyingi mojawapo ni njaa, ukosefu wa makazi bora, ni kuugua na kushindwa kumuona daktari na kupata dawa, ni kukosa kwenda shule na kushindwa kusoma na kuandika.

Umaskini unaendana na kukosa kazi au ajira kwa ujumla lakini pia ni hofu ya siku zijazo au ya kesho kwa vile watu wanashindwa kujua itakuwaje hapo baadaye na wanachofanya ni kuishi siku moja au leo kwavile hakuna mpango wa kesho au wa miaka ijayo.

Ndiyo maana Watanzania wanaathirika na mafuriko umaskini. Serikali na wapanga mipango ya maendeleo wakumbuke kuwa athari za kiuchumi na mateso kwa binadamu zinazotokana na majanga zinaweza kupunguzwa kwa kiasi cha asilimia 60.

Ripoti ya mwaka 2016 ya Benki ya Dunia (WB) inagundua kuwa athari za majanga ya asili hulazimisha watu milioni 26 kuwa maskini kila mwaka (taarifa za wakati huo).

Zaidi ya kuwasukuma watu katika umaskini, athari za maafa kwa ustawi wa binadamu ni kubwa mno na zinazoendelea kuvuruga uchumi na maendeleo ya kizazi cha sasa na kijacho.

Maafa huleta vifo vinavyoacha simanzi, watu kukosa makazi, chakula, elimu na matibabu . Wanachohitaji ni faraja na usalama, utulivu, chakula na kusaidiwa kiuchumi ili kupunguza athari za muda mrefu za maafa, ni vyema mipango inapowekwa taifa likumbuke kuwa wameingia kwenye janga hilo kutokana na umaskini.

Kituo cha Kimataifa cha Kupunguza na Kuokoa wanaopata Maafa (Global Facility for Disaster Reduction and Recovery) na Benki ya Dunia, zinasema madhara ya umaskini kwa watu wanaokumbwa na majanga yanakwenda mbali zaidi ya yale ya kiuchumi pekee.

**ATHARI NI KUBWA**

Mafuriko yanapokumba maskini wanapoteza kila kitu, hasa kile kidogo walicho nacho kuanzia watoto, wenza, mavazi, chakula na nguvu za mwili na uwezo wa akili.

Kuna madhara ya haraka na wakati mwingine yasiyoweza kurekebishwa kwa afya zao hasa athari za kisaikolojia, uchungu na maumivu ya kuwaza hali zao na janga lililowakuta.

Inamaanisha kuwa hata kama mama alikuwa mjamzito akiathiriwa na mafuriko atajifungua mtoto mwenye upungufu wa uzito, kimo kifupi na uwezo wa kiakili ulioharibika au kuathirika.

**KUWASAIDIA**

Japo siyo vibaya kuwasaidia kwa kuwaambia waondoke milimani, mabondeni, kando ya mito na mikondo ya maji , suala la kuwapa makazi kwa muda ni hitaji la awali la usaidizi wa Lakini pia wanahitaji ufumbuzi wa kudumu baada ya janga, ambalo ni kugharamia maendeleo yao kiuchumi.

Wanahitaji kusaidiwa kiuchumi ili kukuza kiwango chao kimapato ikibidi na halmashauri zao, wawezeshwe kupata ajira na kujiajiri ili idadi ya watu wanaoweza kufanya kazi iwajibike na kuondoa umaskini.

Ni muhimu kusaidia waathirika kwa kuwawezesha kuanza biashara ndogo hasa zile zinazomilikiwa na wanawake ili kuzitoa familia katika umaskini na kupunguza athari za muda mrefu za maafa kwa watu hao wanaokumbwa na mafuriko mara kwa mara.

**MAKAZI NAFUU**

Njia mojawapo ya kupunguza vifo vya mafuriko ni kugharamia miradi ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Ni jukumu la serikali kuweka makazi nafuu na kuwapa wakazi wa mabondeni kipaumbele.

Kama taifa linaweza kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji na miradi ya kiuchumi ni wazi kuwa Watanzania wanaoishi mabondeni wanastahili pia kutengewa ardhi na halmashauri zao ili waanze maisha.

Kuna maeneo mengi ambayo inawezekana kujenga nyumba na kuwapa waathirika hao. Lakini pia na kuwawezesha kiuchumi kwenye biashara ndogo ili waweze kulipa na kumiliki nyumba hizo siku zijazo.

Lakini, pia ni jukumu la serikali kugharamia na kuwapa ardhi ili wajenge makazi badala ya kuachwa kufa mabondeni kwa maonyo kwamba kuwa walifuata mito na mikondo ya maji.

Ni wakati pia wa kuandaa maeneo au makazi nafuu na salama kwa wananchi wa mabondeni, milimani na wanaoishi sehemu hatarishi ili waishi kwenye makazi ya bei nafuu, pia kwenye usafiri nafuu, chakula, maji na huduma za afya ili kuwahudumia Watanzania hawa ambao ni wahitaji, wakiwamo watoto na wahitaji hasa wenye ulemavu, wanaoishi na magonjwa sugu na wazee.



## HABARI DODOMA

### DC atangaza operesheni kamata wazazi waliofícha watoto

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali, ametangaza operesheni maalum ya kuwakamata wazazi na walezi wenye watoto waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu lakini bado hawajaripoti shuleni.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao kazi na wakuu wa idara, watendaji kata, vijiji, maofisa tarafa pamoja na wakuu wa shule.

"Kamata kila mzazi, mlezi mwenye mtoto aliyefaulu na hajajiunga kidato cha kwanza mpaka sasa na mtu yeyote atakayekwamisha zoezi hili naye akamatwe," alisema.

Machali alisema serikali inataka kuona kila mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga sekondari hata kama hana sare wasome wapelekwe shule na kusoma kwa muda wa mwezi mmoja.

Alisema kama itafika Jumatatu wiki ijayo wanafunzi watakuwa hawajaripoti shule, Mtendaji wa Kata, Kijiji, Ofisa Tarafa na wakuu wa shule watawajibika wao kwa kupigwa pingu.

Aidha, Machali alisema kufikia Januari 25, mwaka huu kila mtumishi awe anaishi katika kituo chake cha kazi kabla ya kuanza kwa operesheni kali Januari 28 mwaka huu ya kubaini watumishi watakaoshindwa kutekeleza agizo hilo ili wachukulie hatua kali.

**Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao kazi na wakuu wa idara, watendaji kata, vijiji, maofisa tarafa pamoja na wakuu wa shule.**

# Bashungwa kuwashtaki makandarasi wababaishaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amesema anapanga kukutana na Balozi wa China nchini Tanzania ili kumpatia orodha ya majina ya kampuni za makandarasi wababaishaji kutoka nchi hiyo ambao ni kikwazo cha miradi mingi kushindwa kukamilika kwa wakati.

Bashungwa, alisema hayo juzi jijini hapa baada ya kukamilisha ziara yake ya kukagua miradi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara mkoani hapa.

Alisema, ameshaomba nafasi ya kukutana na Balozi wa China nchini ili kumpelekea majina ya makandarasi wa taifa hilo wanaopata zabuni kutoka serikalini na kushindwa kutekeleza miradi kwa wakati na kwa mujibu wa mkataba.

"Nitakutana na Balozi wa China ili kumpelekea majina ya kampuni za makandarasi ambazo zimekuwa zikifanya ubabaishaji kwenye miradi ambayo wamekuwa wakipatiwa na serikali yetu kwa ajili ya utekelezaji," alisema Bashungwa.

Alisema licha ya urafiki uliopo baini ya China na Tanzania, ipo haja ya kampuni hizo ambazo zimeshindwa kutekeleza miradi kwa wakati, kuchukuliwa hatua ikiwa pamoja na kunyimwa zabuni. "Kweli hawa China ni rafiki zetu wa muda na tumekuwa tukiwapa zabuni mbalimbali ambazo zimegharimu kiasi kikubwa cha fedha sasa nitamweleza balozi ili aone nini atafanya kuhusu hizi kampuni," alisisitiza.

Aidha, aliuagiza uongozi wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), kutozipatia miradi mipya kampuni ambazo hazijafika asilimia 60 ya utekelezaji wa miradi yao ya zamani.

Akiwa katika ziara yake jijini Dodoma, Bashungwa alimwagiza Mkandarasi wa Kampuni ya CHICO kutoka nchini China, anayejenga barabara ya makutano ya Ntyuka - Mvumi - Makutano ya Kikombo yenye urefu kilometa 76. Barabara ya Chololo - Mapinduzi (Makao Makuu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi - TPDF) yenye urefu wa kilometa tano, kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha mradi huo unapiga hatua katika utekelezaji wake ifikapo mwishoni mwa mwezi Februari, mwaka huu," alisema.

Kadhalika, alimwagiza mkandarasi huyo kumaliza ujenzi wa sehemu ya barabara ya Kikombo - Makao Makuu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi - TPDF yenye urefu wa Kilomita 16, katika kipindi kilichopangwa.

"TANROADS msimamieni huyu CHICO afanye kazi usiku na mchana, sitaki kuona ucheleweshaji wa mradi huu kwa sababu ya fedha, kuna miradi ambayo wakandarasi wake wanadai fedha, lakini bado inaendelea," alisema Bashungwa.

Vilevile, alisema amechukizwa na kusuasua kwa miradi husani inayofadhiliwa na wadau wa maendeleo kutokana na fedha za utekelezaji zipo na kusisitiza miradi kuendelea kutekelezwa kwa mujibu wa mikataba na kukamilika kwa wakati na kwa ubora.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Colman Gaston, alisema hadi Januari 15, 2024 utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 47 ikilinganishwa na asilimia 81 za mpango kazi wa mkandarasi ambaye yuko nyuma kwa asilimia 34.

Alisema TANROADS Mkoa wa Dodoma, imeweka utaratibu wa usimamizi na ukaguzi wa mradi huo mara kwa mara pia imeweka wahandisi wawakilishi wa mwajiri (Counterpart staff) ambao wapo muda wote wa kazi kuhakikisha kazi zinafanyika kwa viwango vinavyotakiwa na ubora elekezi kulingana na mkataba.

Kaimu Mkurugenzi wa miradi kutoka TANROADS, Mhandisi Jephason Nko, alisema wamejipanga kusimamia miradi ya nchi nzima kujengwa kwa kuzingatia ubora.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alimwahidi Waziri Bashungwa kuwa wataitunza miundombinu ya barabara na miradi mingine kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi kuitekeleza.



Katibu Mkuu wa Chma Cha Mapinduzi (CCM) Dk Emanuel Nchimbi akiingia ofisi za makao makuu ya chama hicho Jijini Dodoma jana alipokaribishwa mara ya kwanza tangu kuteuliwa kushika nafasi hiyo mapema mwaka huu. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# TANESCO yajivunia utekelezaji miradi ya mkakati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Dodoma limetekeleza miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa njia mahususi ya umeme yenye msongo wa kilovoti 33 kwa ajili ya Mji wa Serikali Mtumba na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamini Mkapa (BMH) uliogharimu Sh. Bilioni 2.8.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Dodoma, Donasiano Shamba alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu miradi ya kimkakati iliyotekelezwa na inayotekelezwa jijini hapa.

Alisema mradi mwingine ni wa uhamishaji njia mahusus ya kupeleka umeme katika kituo cha kupozea umeme cha Mzakwe kinachohudumia mashine za kusukuma maji.

Shamba alisema mashine hizo ni za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) ambapo gharama ya mradi huo ni Sh. milioni 700 na umekamilika kwa asilimia 100.

Alisema mradi mwingine ni wa upanuzi wa kituo cha kupoozea umeme cha Mzakwe (33/11KV) kutoka MVA 15 hadi MVA 30 kwa kuongeza njia na transfoma nyingine ambao umegharimu Sh. bilioni 3.4.

"Mradi mwingine ni wa usimamizi wa mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili wenye thamani ya Sh. bilioni 70.4 na mradi wa kupeleka njia mahsusi ya umeme kiwanda cha mbolea Itracom eneo la Nala yenye urefu wa kilomita 25.5 kwa gharama ya Sh. bil.3.5" alisema

Meneja huyo alisema mradi mwingine ni upelekaji njia mahsusi ya umeme katika mitambo ya DUWASA ya kusambazia maji iliyopo eneo la Maili Mbili uligharimu Sh. milioni 735.

"Pia upo mradi wa usimamizi wa mradi wa ujazilizi 2A wenye thamani ya Sh. bilioni 54.49 ambao umeshakamilika na mradi mwingine ni usimamizi wa mradi wa usambazaji wa umeme maeneo ya pembezoni mwa miji wenye thamani ya Sh. bilioni 17.3" alisema.

Alisema mradi mwingine ni wa kupeleka umeme katika vituo vya afya na visima vya maji wa UVIKO-19 wenye thamani ya Sh. bilioni 1.02.

Alisema mradi huo unalenga kupeleka umeme katika vituo vya afya vitano na visima vya maji 29 katika Mkoa wa Dodoma.

Alisema mradi huo unatekelezwa na mkandarasi mzawa Dieynem Co. Ltd ya DSM na umekamilika kwa asilimia 100 Desemba 31, mwaka jana.

Vilevile alisema mradi mwingine ni wa kupeleka umeme kwenye migodi midogo na mashamba ya umwagiliaji katika Mkoa wa Dodoma wa Sh. bilioni 4.06.

Alisema mradi huo unahusisha ujenzi wa miundombinu ya msongo wa kati wa kilovoti 33 umbali wa kilomita 58.5 na kuhusisha kilomita 22 za msongo mdogo, ufungaji wa transfoma 16 na uunganishaji wa wateja 410 katika migodi 13 iliyopo katika Mkoa wa Dodoma.



# RC Njombe aagiza kufukuzwa w’biashara wakaidi sokoni

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

SERIKALI mkoani Njombe imeagiza kufukuzwa kwa wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao kwenye Soko Kuu la Makambako ambao hawataki kuwapeleka watoto katika kituo cha kulelea watoto kilichopo sokoni hapo.

Inadaiwa kuwa wafanyabiashara hao wanashinda na watoto kwenye shughuli zao hali inayohatarisha usalama wao.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alitoa agizo hilo alipofanya mkutano na wafanyabiashara sokoni hapo kwa lengo la kusikiliza changamoto na kero mbalimbali na kuzipatia ufumbuzi.

Mtaka alisema Rais Samia Suluhu Hassan alielekeza kujengwa kwa kituo hicho kwa maslahi yao, lakini wengine wamekaidi kuwapeleka watoto.

“Inakuaje mzazi mjinga ambaye meza ipo chini, juu kuna sehemu ya kutunza mtoto wako kwa salama na mtoto anapewa chakula lishe kizuri kuliko ungemuacha nyumbani na mtoto anakaa sehemu ya darasa anajifunza na watu wa kumfundisha wapo,” alisema Mtaka.

Aidha Mtaka alisema: “Sasa meneja unisikilize kama kuna mtu anamtoto humu ndani na hataki kumpeleka mtoto huko juu atoke kwenye soko, hatuwezi kuleana kwa sababu amekuja Rais Samia hapa mmelalamika nyinyi wenyewe mnataka sehemu ya kuweka mtoto, sasa sehemu imeandaliwa hamtaki kupeleka watoto”.

Awali Meneja wa Soko Kuu la Njombe, Lusajo Mwakiluma alisema Sh. 2,000 kwa siku kimekuwa kikwazo kikubwa kupeleka watoto kwenye kituo hicho ilihali gharama wanazotumia kulea watoto hao nje ya soko ni kubwa zaidi, jambo linaloweza kusababisha mlipuko wa magonjwa pindi wanapokuwa na watoto kwenye biashara zao.

Hata hivyo baadhi ya wafanyabiashara walieleza kero mbalimbali ikiwemo changamoto ya kukosa wateja kutokana na kituo cha mabasi cha zamani kutotumika kwa kushusha wala kupakia abiria.

“Magari kutoka vijijini yaruhusiwe kushusha stendi ya zamani kwa sababu watu kutoka vijijini ndiyo wanaotustawishia uchumi wa soko kuu, kwa sababu tunaagiza bidhaa kutoka soko kuu kwenda vijijini,” alisema Joram Sanga.

Mfanyabiashara mwingine, Frola Chaula aliiomba serikali kuboresha mfumo wa majitaka katika soko hilo kwa sababu hakuna hali inayosababisha wafanyabiashara kumwaga maji mahala ambako sio rasmi.



Kundi la ng’ombe lililokuwa likichungwa pembezoni mwa Mto Zira uliopo wilayani Chunya likiwa limetelekezwa na mchungaji mwishoni mwa wiki ambaye alijificha baada ya kuwaona maofisa wa Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini (NEMC). **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Wachimbaji madini 100 wapewa leseni za kuchimba mtoni

**Na Nebart Msokwa,**
CHUNYA

MTO Zira uliopo wilayani Chunya mkoani Mbeya uko hatarini kutoweka kutokana na zaidi ya wachimbaji wa madini 100 kupatiwa leseni za kuchimba ndani ya mto huo.

Mto huo ni miongoni mwa mito inayomwaga maji ndani ya Ziwa Rukwa na unategemewa na wananchi wanaoishi kwenye baadhi ya kata za wilaya za Chunya na Songwe.

Kutokana na hali hiyo, serikali imeagiza wataalamu wa mazingira kutoka Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kufanya tathmini ya kina kuhusu athari za kimazingira zitokanazo na uchimbaji madini kwenye mto huo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Seleman Jaffo alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua eneo hilo kwa lengo la kujiridhisha baada ya kubaini idadi kubwa ya wachimbaji wakiomba leseni za kuchimba.

“Sitaruhusu uchimbaji kuendelea katika mto huu mpaka wataalamu wangu wakamilishe tathmini ya athari za kimazingira, mto huu una utajiri mwingi wa dhahabu ndio maana tumepokea maombi mengi kutoka kwa wawekezaji lakini lazima kwanza tulinde mazingira yetu,”alisema Jaffo.

Aliagiza wataaalamu hao kukaa pamoja na kujadili kilicho sahihi kifanyike ikiwa ni pamoja na kutoa masharti maalumu kwa wawekezaji ya kulinda mazingira ikiwemo kuainisha teknolojia ya aina gani itumike kwenye uchimbaji ambayo ni salama kwa uhifadhi wa mazingira pamoja na shughuli za uchenjuaji kufanyike nje ya mto ili kulinda mazingira.

Alisema serikali inahitaji wawekezaji kwa ajili ya kuinua Uchumi lakini wanahitaji wawekezaji watakaofuata taratibu za utunzaji wa mazingira ili kulinda vyanzo vya maji kwa ajili ya kuepukana na athari zitokanazo na ukame.

Alisistiza wawekezaji wa migodi nchini kuhakikisha wanakuwa na wataalamu wa mazingira ili wawashauri namna bora ya kulinda mazingira.

Mkurugenzi wa utekelezaji na uzingatiaji wa sheria kutoka NEMC, Thobias Richard alisema lengo la baraza hilo ni kuchochea uwekezaji unaolinda mazingira ya sasa na baadaye, hivyo hawapo tayari kuendelea na wawekezaji wanaokiuka masharti ya uhifadhi wa mazingira.

Alisema awali walifika katika eneo hilo na baada ya kukagua walibaini mwekezaji hakutekeleza masharti ya kibali alichopewa ikiwemo kufanya tathmini ya athari za mazingira kwa kushirikisha mamlaka husika pamoja na wananchi.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa kimadini Chunya, Mhandisi Laurent Mayala alisema hadi sasa wametoa leseni zaidi ya 100 kwa wawekezaji walioomba kufanya shughuli za uchimbaji katika eneo la mto huo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Chunya, Noel Chiwanga alisema suala la uharibifu wa mazingira katika mto huo halikwepeki kwa sababu dhahabu iko katikati ya maji, hivyo hofu yao ni kuchafuliwa kwa vyanzo vya maji.

Hivyo alipongeza uamuzi wa serikali wa kufanya tathmini upya kabla ya kuruhusu shughuli za uchimbaji.

## Wananchi watakiwa kuwasapoti wahisani wanaojitokeza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI jijini Mbeya wametakiwa kuwaunga mkono wahisani wanaojitokeza kuwasaidia mahitaji ya shule wanafunzi wanaotoka kwenye mazingira magumu.

Aidha wazazi na walezi wametakiwa kuwafundisha watoto wao kuwa na utaratibu wa kushukuru pale wanaposaidiwa ili kutengeneza mazingira ya kusaidiwa tena wakati mwingine.

Diwani wa Kata ya Iyela, Mussa Ismaily alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya kuchangia mahitaji ya shule kwa wanafunzi 30 wa shule za msingi katika Kata ya Iyela, iliyoandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Child care and Youth Empowerment Tanzania (CHICAYETA).

Alisema kumekuwa na baadhi ya watu wanaowakatisha tamaa wahisani wanaojitolea kusaidia watu wasioweza kwa kudhani wanatoa misaada hiyo kwa lengo la kujinufaisha, hali ambayo imekuwa ikiwavunja moyo baadhi yao na kuacha kuendelea kusaidia jamii ya wasiojiweza.

“Tuache hii tabia ya kusema wanatupatia kidogo wao wananufaika na vingi au wanachangisha fedha ili wapate ulaji, ndugu zangu kauli hizi zimekuwa zikikwamisha jitihada za wahisani wetu kuendelea kusaidia wahitaji, hata serikali imefanya mengi lakini tunalalamikia kila jambo niwaombe tuwe na shukrani kwa tunachokipata,” alisema Mussa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa Shirika la SAMAFO, Tabitha Bugali aliwataka wazazi na walezi kuheshimu misaada waliyopewa kwa ajili ya watoto wao kwani wahisani wamejitoa kwa hali na mali kusaidia watoto hao ili kuwapa faida ya baadae na sio wao kupata faida.

Hivyo aliwataka wazazi na walezi kuwalinda watoto wao kwa kuhakikisha wanafuatilia na kuwachunguza hali zao mara kwa mara, huku akiwataka kutowaamini wageni wanaowakaribisha nyumbani hata kama ni ndugu zao.

Mkurugenzi wa CHICAYETA, Abigael Abdallah, alisema taasisi hiyo inalenga kuwasaidia watoto wanaotoka katika familia zisizomudu mahitaji kupitia michango mbalimbali ya wadau ili ikiwa ni upendo wa kujitoa kwa watu wengine ili kuwasaidia kufikia maendeleo na ustawi wa jamii na kiuchumi.

Alisema watoto waliopatiwa mahitaji kati yao ni yatima wengine wanaishi na mzazi mmoja na wengine wanatoka familia zisizo na uwezo wa kumudu mahitaji ya kila siku.





## Serikali kukusanya Trilioni 3.38/- mwaka wa fedha 2024/25

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Dk.Juma Malik Akil amesema Serikali ya Zanzibar inatarajia kukusanya Sh. trilioni 3.38 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 548.

Akiwasilisha hotuba ya ufunguzi wa jukwaa la uchumi na bajeti kwa mamlaka za serikali za mitaa Wilaya ya Mjini, Dk. Malik alisema ifikapo Julai mwaka huu serikali imepanga kukusanya Sh. trilioni 2.838 za makusanyo sawa na asilimia 99 kwa mwaka 2023/2024.

Alisema kwa mwaka 2024/2025 serikali inatarajia kupokea watalii 8,290,000 kutoka watalii 6,380,000 wa mwaka 2023/2024.

Alisema mafanikio hayo yamefikiwa kutokana na kuwepo kwa mpango nzuri wa uhamasishaji kodi kwa taasisi zinazohusika na ukusanyaji wa fedha kiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) pamoja na sekta zinazohusika na utalii.

"Juhudi zinazochukukiwa na taasisi zetu za kuhimiza kodi kwa hiari kwa wafanyabiashara imesaidia kuongezeka kwa mapato ya serikali," alisema.

Katibu huyo alisema kuwa kupatikana kwa fedha hizo serikali imeimarisha miundombinu ya majengo ya aina mbalimbali ikiwemo afya, elimu, barabara na maeneo mengine kwa kutumia fedha hizo.

Sambamba na hayo alisema serikali inatarajia kuongeza ushirikiano na taasisi za kodi kuona fedha zilizopangwa kukusanywa zinafikiwa kwa wakati uliopangwa.

Alisema mapato yameongezeka kwa taasisi na sekta ikiwemo Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na serikali itaendelea kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari pamoja na kuimarisha mazingira bora ya biashara.

Akifungua jukwaa hilo, Waziri wa Nchi, Ofisi, ya Rais Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alizitaka taasisi zinazokusanya mapato kutumia vyema mifumo ili kuondosha changamoto ya upotevu wa mapato.

Aidha Dk. Saada alisema zipo taasisi ambazo bado hazijaweka vyema mifumo na kusababisha kupoteza mapato na kuwataka washiriki wa jukwaa hilo kutoa maoni na mipango ambayo yatasaidia usimamizi wa mapato ya umma kwenye serikali za mitaa.

# Elimu usalama na afya kazini kuendelea kutolewa ZNZ

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA Mafunzo kutoka kitengo cha idara ya usalama kazini, Khairat Omar Rajab, amesema wataendelea kutoa elimu ya usalama na afya kazini ili kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa na afya bora wakati wote wanapokuwa katika majukumu yao ya kazi.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza katika tamasha la maonesho lililowashirikisha wajasiriamali, wafanyabiashara pamoja na taasisi za serikali na binafsi Nyamanzi Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja.

Alisema lengo la kushiriki katika maonesho hayo ni kutoa taaluma zaidi ya masuala ya usalama na afya kazini na kuelimisha jamii juu ya kazi zinazofanywa na idara hiyo.

Ofisa huyo alisema kuwa idara ya usalama na afya kazini ipo kwa mujibu wa Sheria Namba 8 ya Mwaka 2005 ambapo pamoja na mambo mengine taasisi hiyo ina jukumu la kuhakikisha mazingira ya kazi yanakuwa salama na vihatarishi vyote vinavyoweza kusababisha wafanyakazi kupata madhara vinaondoka katika maeneo ya kazi.

Hata hivyo alisema dhamira kuu ya idara hiyo ni kuimarisha usalama na afya katika sehemu za kazi pamoja na kuendelea kutoa elimu katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba hatua ambayo itasaidia jamii kufahamu umuhimu wa afya na usalama kazini.

Alisema hatua hiyo itasaidia kunyanyua hali za maisha ya wafanyakazi kuwa na kazi zenye staha na maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Aidha alitumia fursa hiyo kuwasisitiza waajiri kusajili maeneo yao ya kazi, kuzingatia muhimu wa masuala ya usalama na afya kazini na waajiriwa kufahamu kuona umuhimu wa matumizi ya vifaa vya kinga wanavyopewa na waajiri wao.

Wakizungumza baadhi ya wananchi na wanafunzi wa vyuo vikuu, waliofika katika maonesho hayo na kutembelea banda ldara hiyo walisema elimu waliyopatiwa na maofisa hao ni muhimu na itawasaidia kufahamu umuhimu wa kujikinga na madhara yatokanayo katika sehemu za kazi.



Sehemu ya daraja la mto Tegeta jijini Dar es Salaam lililobomoka kutokana na mvua kubwa iliyonyesha juzi likifanyiwa ukarabati jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mahakama ya Rufani kujengwa Kisiwani Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAHAKAMA ya Rufani Tanzania inatarajia kujenga jengo la mahakama Kisiwani Pemba ambalo litakuwa na huduma za utatuaji na upatikanaji wa haki.

Hayo yalisema jana visiwani Zanzibar na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dk. Khatibu Kazungu katika mkutano wa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

Akisoma maazimio ya kikao hicho mbele ya mawaziri wa Katiba na Sheria na Katiba wa SMT na SMZ katibu mkuu huyo alisema Mahakama ya Rufani ina masjala yake Zanzibar lakini kikao kimeona kwamba vikao vingi vya mahakama hiyo vinafanyika Unguja ikilinganishwa na Pemba.

Hivyo alisema kwa vile idadi ya vikao vya mahakama hiyo Pemba ni vichache na baada ya kugundulika changamoto hiyo Mahakama ya Rufani imepanga kujenga jengo la mahakama Pemba, ujenzi huo unatarajiwa kuanza Februari mwaka huu.

"Lakini waheshimiwa mawaziri tulitaarifiwa kwamba pande zote mbili za muungano kati ya Mahakama ya Tanzania na ya Zanzibar, ushirikiano ni mzuri na kumekuwa na vikao mbalimbali vya kushughulikia changamoto ambazo zinakabili mahakama hizi," alisema Kazungu.

Alisema baadhi ya ushirikiano huo ni katika eneo la mfumo wa uendeshaji wa kesi kielektronik kwa kujengeana uwezo na kukutana mara kwa mara kujadiliana namna ya kuboresha maeneo hayo.

Aidha katika kakikao hicho viongozi hao walitoa taarifa kuhusu maandalizi ya mkutano wa mawaziri wa sheria wa Jumuiya ya Madola unaotarajiwa kufanyika visiwani Zanzibar Machi 4 mwaka huu.

Alisema kuwa katika hilo maandalizi yapo vizuri na wameshaunda kamati za kufuatilia na kupanga bajeti ya Sh. bilioni 2.9 kwa ajili ya kuwezesha kikao hicho.

Naye Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana na Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman waliwataka watendaji wa wizara hizo kuwashirikisha mawaziri wao kwa yale mambo ambayo yatapaswa kuyafahamu.

Walisema ushirikishwaji wa mawaziri inasaidia kwa sababu wao wamekuwa wakiingia katika vikao mbalimbali na kuvielezea na kutolewa ufumbuzi.

Katika kikao cha awali ambacho kilishirikisha watendaji pekee wa wizara hiyo kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Nchi , Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala bora maadhimio 10 yaliwasilishwa na kupitia na .

Baadhi ya maadhimio hayo ni taasisi zote za sheria za pande mbili za muungano ziandae hati za makubaliano kwa ajili ya kuimarisha ushirikiano, wataalamu wa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Zanzibar na Bara wakajifunze katika uendeshaji wa masuala ya mashtaka na makosa ya uhalifu wa kupangwa kwa sababu imeonekana bara kuna udhoefu mzuri kwenye eneo hilo.

Pia wigo wa utafiti uliofanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania kuhusu udhalilishaji uongezwe na kuhusisha Zanzibar ili matokeo hayo yasaidie kiboresha udhibiti wa makosa ya udhalilishaji na wataalamu wa pande mbili wa sheria, washirikiane katika kuandaa ushahidi na maelezo wa kesi za kimataifa za madai zinazotatuliwa kwa utaratibu wa usuluhishi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**HURA RAMADHANI CHUU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne na darasa la saba, cheti cha kidato cha nne chenye index No. **S2483/0016** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KOLO SECONDARY SCHOOL mwaka 2020, Vyeti hivi vimepotea mkoani Dodoma. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya Polisi: PHQ/ **DOD/DOD/270/2024.**

## KUPOTELEWA KADI YA PIKIPIKI

**Anjela Samson Dotto** anatangaza kupotelewa na Kadi ya Pikipiki aina ya **SANLG** yenye namba za usajili **MC 198 CZH,** injini no **157FM121910631.** Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Angela kwa simu namba **0768-869494.**
Taarifa ya Polisi
**PHQ/SHI/SHI/234/2024.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 597 LA 2023**
**NNAMUGINGA G. MAJELLA……MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**

- **JULIUS PETER**
- **FLORA ALEXANDER LYIMO….MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

- **JULIUS PETER**
- **FLORA ALEXANDER LYIMO –**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**
**NNAMUGINGA G. MAJELLA** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 22/2/2024 saa 03:00 Asubuhi/Mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 17 Mwezi 01, 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA
DAR ES SALAAM
SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA. 248 YA 2020

KABULA AZARIA NG'ONDI
ADIEL KUNDASENY MUSHI
NEEMA ADIEL MUSHI
SIMON PAUL MEELA ……………………WARUFANI

DHIDI YA

MARIA FRANCIS ZUMBA
MSOLPA INVESTMENTS LIMITED ……………WAJIBU RUFANI

KWA:
MSOLOPA INVESTMENT LIMITED

POPOTE MLIPO

Mnajulishwa kwamba shauri la Rufaa ya Madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii hapa Dar es Salaam tarehe 6/2/2024 saa tatu kamili asubuhi (9:00).

Mnapewa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyinyi wenyewe au mwakilishi wenu anayetambulika kisheria basi rufaa itasikilizwa bila ya uwepo wenu.

Imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 19/1/2024.

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

J. J. KAMALA
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo KAWE Wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KAWE Mkoa DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai/Ndoa Na. 07, 2024**

**Jina la Mdai NICKSON JACKSON KAWICHE**

**Jina la Mdaiwa…………..**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: TUMAINI LEMA NA AMANI URASA – GOBA DAR ES SALAAM**
Kwa kuwa Mdai/Wadaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba K**UJA KUJIBU MADAI YA PESA SH. 2,380,000/ ILIYOFUNGULIWA HAPA MAHAKAMANI**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 25 Mwezi 02 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
Angalizo: Kama hautahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 22 Mwezi 01 Mwaka 2024.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE

## MARUDIO YA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICES LTD, DENNESTO COMPANY LIMITED** tunautangazia umma kuwa tunarudia mnada wa hadhara wa kuuza mali ya mdaiwa kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdaiwa | Dalali | Aina ya Mali /Mahali | Tarehe mnada |
|---|---|---|---|
| Vicent Ringson Mberesero | DENNESTO COMPANY LIMITED | Mitsubishi Canter T.682 DUC, Makumbusho Yard- Dar | 30 Jan 2024 |

**Masharti ya Mnada**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.

Gharama za kukagua na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: - DENNESTO- 058896226/070769777826**


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Hamas wakiri makosa uvamizi Israel

**GAZA, Palestina**

KUNDI la Hamas limetoa ripoti ikielezea shambulio la kusini mwa Israel kama hatua ya lazima na jibu la kawaida huku likikiri makosa katika utekelezaji wake wa uvamizi, na kutoa pendekezo la kusitisha vita hivyo hatua ambayo imepingwa vikali na Israel.

Akizungumza jana Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu alionyesha msimamo wa kukataa pendekezo la Hamas la kusitisha vita na kuwaachilia mateka ili kubadilishana, kuondoa majeshi ya Israel, kuwaachilia wafungwa na kukubali utawala wa kundi linalojihami la Gaza.

Netanyahu, ambaye anakabiliwa na shinikizo la ndani la kuwarudisha mateka nyumbani, alisema kwamba kukubali masharti ya Hamas kutamaanisha kuwaacha kundi lenye silaha na kwamba wanajeshi wa Israel watakuwa wameanguka bure.

"Ninakataa kabisa masharti ya kujisalimisha kwa wanyama wakubwa wa Hamas, tukikubali hili hatutaweza kuwahakikishia raia wetu usalama, hatutaweza kuwarejesha watu waliohama nyumbani salama na Oktoba saba ijayo itakuwa ni suala la muda tu," alisema Netanyahu.

Inaelezwa kuwa awali Netanyahu alirudia upinzani wake dhidi ya taifa huru la Palestina, akisisitiza kuwa hatakubali udhibiti kamili wa usalama wa Israel katika eneo lote la magharibi mwa Jordan.

Netanyahu yuko chini ya shinikizo kwa pande nyingi, huku familia za mateka zikitaka kufikiwe makubaliano ya kurejesha wapendwa wao, wanachama wa muungano wake wa siasa kali za mrengo wa kulia wanashinikiza kuongezeka kwa vita, na tofauti zinazoongezeka zinagubika uhusiano na utawala wa Rais wa Marekani Joe Biden.

Siku chache zilizopita, Jukwaa la Mateka na Familia Zilizotoweka lilianza maandamano nje ya nyumba ya kibinafsi ya kiongozi wa Israeli huko Jerusalem, na kuahidi kutoondoka hadi atakapokubali makubaliano ya kuachiliwa kwa mateka.

Kupitia taarifa iliyotolewa na kundi hilo, ilisema ikiwa waziri mkuu ataamua kuwatoa mhanga mateka, anapaswa kuonyesha uongozi na kushiriki kwa uaminifu msimamo wake na umma wa Israel.

Hamdah Salhut wa Al Jazeera, akiripoti kutoka Jerusalem Mashariki inayokaliwa, alisema kuwa waandamanaji wanahisi hawaonekani au kusikilizwa na serikali yao.

"Wanahisi kupuuzwa na kusahauliwa, pia mmetofautiana kutoka ndani ya baraza la mawaziri la vita mjumbe mmoja akisema kwamba labda kushindwa kabisa kwa Hamas sio lengo la kweli kwa serikali kulenga na kwamba lazima pia uchaguzi ufanyike, ili umma uonyeshe maoni yao na imani kwa serikali," alisema.

Aidha, inaelezwa kuwa Hamas iliwaachia huru zaidi ya wafungwa 100 ili kuachiliwa huru wafungwa 240 wa Kipalestina kama sehemu ya mapatano mafupi yaliyoandaliwa mwishoni mwa mwezi Novemba na Misri, Qatar na Marekani.

Hamas bado inawashikilia watu 136 mateka, kwa mujibu wa maofisa wa Israel. Huku ikielezwa kuwa takriban Wapalestina 25,105 wameuawa huko Gaza tangu Israel itangaze nia yake ya kuiondoa Hamas kujibu mashambulizi yaliyotekelezwa na kundi hilo Oktoba 7, 2023. **ALJAZEERA**




Gavana wa Jimbo la Florida Ron Desantis kushoto aliyejiengua kwenye kinyang'anyiro cha urais na kumuunga mkono Donald Trump. **PICHA: MTANDAO**

## Trump anyanyuka kisiasa Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

NYOTA imezidi kumuwakia Rais wa zamani wa Marekani Donald Tramp, baada ya Gavana wa Florida Ron Desantis kusimamisha kampeni zake za kuwania urais kupitia chama cha Republican na kumuidhinisha Trump.

Inaelezwa kuwa gavana huyo wa Florida alifikia hatua hiyo siku mbili kabla ya uchaguzi wa mchujo katika jimbo la New Hampshire. Ikielezwa kuwa hiyo inafikisha kikomo azma ya Desantis ya kuingia White House baada ya kushindwa kukidhi vigezo.

Akihutubia siku chache zilizopita katika jimbo la New Hampshire, Gavana Desantis alisema "Ni wazi kwangu kwamba wapiga kura wengi wa mchujo wa chama cha Republican wanataka kumpa Trump nafasi nyingine".

Inaelezwa kuwa Desantis alimdhihaki Balozi wa zamani wa Umoja wa Mataifa Nikki Haley, ambaye kwa muda mrefu alikuwa mpinzani wake wa karibu kwa nafasi ya pili katika kinyang'anyiro cha kutafuta tiketi ya chama hicho, akisema kwamba hafai kuwa rais wa Marekani.

Gavana huyo, ambaye amekuwa akionyesha shauku kubwa, aliingia kwenye kinyang'anyiro cha urais wa 2024 akiwa na matumaini makubwa katika azma yake ya kumshinda Trump, na kura za maoni za awali zilionyesha kwamba alikuwa katika nafasi nzuri ya kufanya hivyo.

Yeye na washirika wake walichangisha zaidi ya dola milioni 100, na alijivunia rekodi yake ya kisheria kuhusu masuala muhimu kwa wahafidhina wengi, kama vile utoaji mimba na mafunzo ya masuala ya rangi na jinsia shuleni.

Hata hivyo inabainishwa kuwa wiki iliyopita alishindwa uchaguzi wa mchujo katika jimbo la Iowa ambao alikuwa ameapa kushinda kwa asilimia 30 kwa Trump.

Vile vile inaelezwa kuwa hatua ya Desantis ya kujiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho sasa inawaacha Trump na gavana wa zamani wa jimbo la South Carolina kushindania nafasi hiyo. **VOA**

## Cameroon yatoa chanjo malaria

**YAOUNDE,** Cameroon

CAMEROON imezindua mpango wa kwanza duniani wa chanjo dhidi ya malaria, katika mapambano ya kimataifa yanayotarajiwa kuokoa maelfu ya maisha ya watoto kote barani Afrika.

Inaelezwa kuwa chanjo ya RTS, iliyoidhinishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), ambayo ilitengenezwa na kampuni ya utengenezaji wa dawa ya Uingereza (GSK), inalenga watoto wachanga katika wilaya 42 zilizoathiriwa zaidi nchini Cameroon.

Inabainishwa kuwa nchi hiyo ya Afrika ya kati itakuwa ya kwanza kutoa dozi kupitia mpango wa kawaida wa chanjo, kufuatia kampeni za majaribio zilizofanikiwa nchini Kenya, Ghana na Malawi.

Hata hivyo inaelezwa kuwa utoaji huo wa chanjo ambao umeanza rasmi jana ulielezwa na maofisa wa afya kama hatua muhimu katika juhudi za miongo kadhaa za kukabiliana na ugonjwa wa malaria barani humo.

Vile vile inaelezwa kwamba nchi nyingine 20 zinalenga kuzindua mpango huo mwaka huu, kulingana na muungano wa kimataifa wa chanjo Gavi. **BBC**

# KITAMBI NA SABABU KUIPELEKA GEITA GOLD KAMBINI MOROGORO

**Na Oliver Albert**

KLABU ya Geita Gold, imeweka kambi mkoani Morogoro ikijiandaa na Ligi Kuu Bara huku Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Dennis Kitambi, akisema mzunguko wa pili anataka mabao mengi na ushindi wa mechi nyingi.

Geita Gold iko nafasi ya 10 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 16 baada ya kucheza michezo 13, imeshinda minne, sare nne na kupoteza michezo mitano.

Kwa mujibu wa Kitambi, idadi ndogo ya mabao waliyofunga katika mechi hizo 13, ndio zimemfanya kuongeza idadi kubwa ya washambuliaji kwenye dirisha dogo la usajili, jambo ambalo limemlazimu kuwa kuingia kambini ili kupata muunganiko mzuri wa kikosi chake.

**Geita imefunga mabao tisa na kuwa timu ya pili iliyofunga mabao machache kwenye ligi sawa na Tabora United na Mashujaa FC, wakati Kagera Sugar ndio kinara wa mabao machache baada ya kufunga mabao nane tu.**

Kitambi alisema wameona wajichimbie Morogoro ili kupata utulivu wa kusahihisha makosa yao ili ligi ikirejea wawe vizuri zaidi.

"Tumeweka kambi Morogoro tukiingia wiki ya pili sasa na tutakuwapo hapa mpaka pale bodi ya ligi itakapotoa msimamo wa ligi itarejea lini tena,@ alisema Kitambi.

Alisema mzunguko wa pili wa ligi wanahitaji kushinda mechi nyingi iwezekanavvyo ili wajiweke salama na ndio maana ameongeza idadi kubwa ya washambuliaji.

"Changamoto yetu kubwa katika mechi zilizopita ilikuwa upande wa kufunga mabao na kumbuka tunaenda mzunguko wa pili, hivyo tunahitaji kufunga sana.

"Mzunguko wa lala salama kila timu inakuwa imejiandaa kutafuta ushindi na kama unavyoona msimamo ulivyo wengi tumeshonana na hatupishani pointi kubwa kiasi kwamba ukipata suluhu ni kitu ambacho hakikusaidii sana, hivyo lazima upambane kushinda tu," alisema Kitambi.

Geita imewaongeza kikosini washambuliaji Francis Bakari kutoka Cameroon, Ramadhan Kapera na Jonathan Ulaya.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa pili kushoto), akipokea Kombe la Mapinduzi kutoka kwa Mfadhili wa Timu ya Mlandege, Abdulsatar Daudi, wakati wa hafla ya chakula cha usiku alichowandalia timu hiyo na Kamati ya Maandalizi ya Sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar juzi Ikulu Zanzibar. Kulia ni rais wa timu ya Mlandege, Kamal Abdulsatar Daudi na kushoto ni Hussein Abdulsatar Daudi. Mlandege ilibeba ubingwa huo kuifunga Simba SC bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa New Amani Complex Januari 13, mwaka huu. **PICHA: IKULU**

# Aiyee ndani Coastal Union ikianza mazoezi

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Coastal Union kimeanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuendelea tena katikati ya mwezi ujao, huku ikimpokea mchezaji wake mpya, Salim Aiyee aliyesajiliwa kutoka Mbuni FC.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Abbas El Sabri, amesema jana kuwa rasmi sasa wanamtangaza Aiyee, straika wa zamani wa Mwadui FC kuwa mchezaji wao baada ya kumalizana na klabu yake ya Mbuni FC inayoshiriki Ligi ya Championship.

Alisema pamoja na kuwapo tetesi nyingi, lakini walishindwa kumtangaza kwa sababu hawakuwa wamemalizana na klabu yake hiyo ambayo ilikuwa na mkataba naye.

"Tayari ameshawasili Tanga na ameshaanza mazoezi, akijiandaa kwa mapambano ya kuisaidia klabu yetu kwenye ndoto yetu ya kushika moja kati ya nafasi nne za juu msimu huu.

Spidi yake ile tunayoijua na mabao yake tunahitaji kuyaona tena Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Ofisa Habari huyo.

Hadi anaondoka Ligi ya Championship, Aiyee alikuwa amepachika mabao tisa kwa michezo 15 aliyocheza na kuiacha timu ya Mbuni FC ikiwa nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Straika huyo anarejea Ligi Kuu baada ya kutikisa msimu wa 2018/19 akiwa na Mwadui FC akishika nafasi ya pili kwenye ufungaji bora akiwa na mabao 18, nyuma ya Meddie Kagere wa Simba aliyekuwa kinara kwa mabao 23, akiwa amewazidi mastraika hatari msimu huo, Heritier Makambo wa Yanga aliyekuwa na mabao 17 na John Bocco aliyemaliza na mabao 16.

El Sabri pia amesema kikosi hicho kimeanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa ligi ambayo kwa sasa imesimama kupisha Fainali za AFCON zinazoendelea nchini Ivory Coast.

"Kikosi chetu kimesharudi kutoka katika mapumziko na tayari kimeshaanza mazoezi katika Uwanja wa Mkwakwani, tunaendelea tulipoishia," alisema.

# Mashujaa FC yajichimbia Dar

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Mashujaa FC kimeweka kambi jijini Dar es Salaam kujiwinda na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara lengo likiwa ni kusaka alama sitau dhidi ya wakongwe wa soka hapa nchini, Simba na Yanga.

Katika mzunguko wa kwanza Mashujaa FC imecheza michezo 12 kati ya mechi hizo haijacheza dhidi ya Simba na Yanga na michezo hiyo ikiwekwa kiporo kutokana timu hizo kongwe kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Mashujaa FC, Mohammed Abdallah (Bares), alisema wameweka kambi Dar es Salaam hadi Februari 7, mwaka huu, watarejea kwenye maskani yao, Kigoma.

Alisema wakiwa Dar es Salaam watakuwa na mechi za kirafiki zisizopungua tatu kwa ajili ya kutengeneza muunganiko kati ya wachezaji wazamani na wapya waliosajiliwa dirisha dogo.

"Hatuko katika nafasi nzuri kwenye msimamo, tunatakiwa kuanza mazoezi mapema kupata muunganiko mzuri, kucheza mechi ya kirafiki nipate mwanga wa kuona mapungufu ya timu yangu na kuyafanyia kazi kabla ligi haijarejea.

"Tuna kazi kubwa ya kuhakikisha duru la pili tunapata matokeo mazuri, kufikia hapo lazima tujiandae mapema kwa sababu kuna mechi ngumu ugenini na nyumbani ikiwamo Simba na Yanga na tunahitaji alama mbele ya hizi timu," alisema Bares.

Aliongeza kuwa wanahitaji kupata matokeo kwenye duru la pili kujiondoa kwenye nafasi ya pili kutoka mkiani mwa msimamo wa ligi hiyo na kujiweka kwenye mazingira ya nafasi za juu ili kutoshuka daraja wala kucheza Play Off mwishoni mwa msimu.

Mashujaa inashika nafasi ya 15 katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa imecheza mechi 12, ikishinda mbili, sare tatu na kufungwa michezo saba, hivyo kukusanya alama tisa tu.

**Wakiwa Dar es Salaam watakuwa na mechi za kirafiki zisizopungua tatu kwa ajili ya kutengeneza muunganiko kati ya wachezaji wazamani na wapya waliosajiliwa dirisha dogo.**

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TONEY HATASHINIKIZA KUSEPA

MSHAMBULIAJI wa Brentford na England, Ivan Toney, ambaye amekuwa akihusishwa na uhamisho wa Arsenal na Chelsea, hatashinikiza kuhama Januari na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anapanga kubaki na 'Nyuki' hao hadi msimu wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### TRIPPIER SASA AGOMEWA

KLABU ya Newcastle United haitawauza wachezaji wake wawili wa England, beki Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 33, anayelengwa na Bayern Munich - au mshambuliaji Callum Wilson (31), ambaye amekuwa akihusishwa na Atletico Madrid, mwezi huu. ***(Telegraph)***

### NEWCASTLE YATANGAZA BEI

NEWCASTLE United wanataka euro milioni 15 kutoka Bayern Munich kwa ajili ya kumuuza Kieran Trippier, wakati klabu hiyo ya Ujerumani inataka tu mkataba wa mkopo. ***(Bild in Sport)***

### BURUNO KUPELEKWA SOKONI

KLABU ya Newcastle United italazimika kuwauza kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26 na mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak (24), ili kukidhi kanuni za haki za kifedha. ***(Football Insider)***

### MOURINHO AITAKA ROMA

JOSE Mourinho anapendelea kusalia Italia baada ya kutimuliwa na as Roma na Mreno huyo anatazamiwa kufanya mazungumzo na rais wa Napoli, Aurelio de Laurentiis kuhusu kuchukua mikoba ya mabingwa hao wa Serie. ***(Times)***

### PALACE YASAKA KOCHA

KLABU ya Crystal Palace imeanza kuandaa orodha fupi ya watu wanaowania kuchukua nafasi ya kocha, Roy Hodgson, huku bosi wa zamani wa Nottingham Forest, Steve Cooper, kocha wa zamani wa Wolves, Julen Lopetegui, bosi wa Ipswich, Kieran McKenna na bosi wa zamani wa Mainz, Bo Svensson wakiwa miongoni mwa wanaotajwa kuwania nafasi hiyo. ***(Mail)***

### SPURS IMEKATAA OFA

KLABU ya Tottenham Hotspur imekataa ofa ya pauni milioni 20 kutoka kwa Al-Nassr kwa ajili ya mlinzi wa Brazil, Emerson Royal mwenye umri wa miaka 25, huku timu hiyo ya Saudi Pro League ikifikiria kuongeza ofa yao. ***(Sport)***

### HOJBJERG AWANIWA JUVE

KLABU ya Juventus bado inavutiwa na kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28, lakini Spurs watazingatia tu mauzo ya kudumu au mkopo na wajibu wa kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Denmark. ***(Sky Sports Germany)***

### GODFREY CHAGUO MILAN

MLINZI wa Everton, Ben Godfrey anaweza kuwa chaguo kwa AC Milan, wakati Sheffield United na Leeds United pia zinavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Calciomercato)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SALAH AIACHA MISRI AFCON, ARUDI LIVER

**Klabu yataka kumfanyia matibabu yenyewe, kurudi kama wakitinga...**

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah anarejea Liverpool kwa ajili ya matibabu ya jeraha la mguu alilopata kwenye michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), lakini Misri wana matumaini kuwa anaweza kurejea kwa hatua ya nusu fainali kama wakifuzu

**Salah alijeruhiwa katika sare ya mabao 2-2 dhidi ya Ghana Alhamisi katika mchezo wa Kundi B.**

"Ina maana kwamba anakuja kufanyiwa matibabu na sisi," alisema Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp juzi, kabla ya Misri kuthibitisha kurejea kwa fowadi huyo.

Misri jana Jumatatu ilikuwa inacheza na Cape Verde ili kutafuta nafasi ya kufuzu hatua ya mtoano.

Awali Shirikisho la Soka la Misri lilisema Ijumaa kwamba fowadi wa Liverpool, Salah angeshiriki tena katika michuano hiyo iwapo taifa lake litafuzu kwa robo fainali itakayopigwa Februari 2 au 3.

Alipoulizwa kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, atarejea Afcon iwapo nchi yake itaendelea, Klopp aliongeza: "Ningesema ikiwa Misri itafuzu kwa fainali, ikiwa yuko fiti kabla ya fainali, basi pengine ndiyo."

Klopp alikuwa amependekeza Ijumaa kwamba tatizo la Salah la misuli ya paja huenda likawa kubwa, ikizingatiwa kuwa fowadi huyo alikuwa amekosa mechi 10 pekee za ligi kwa 'Wekundu' hao katika zaidi ya misimu sita.

"Alishtuka na hakuona kwa nini alipigwa na kitu kikali," alisema Mjerumani huyo.

"Majeraha haya ya misuli ya paja yana njia tofauti. Alihisi hivyo na tunajua ni mara ngapi Mo anatoka nje, au anahitaji kutoka, kwahiyo ni jambo la hakika."

Mara ya mwisho kati ya mataji saba ya Misri kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika ilikuja mwaka 2010, mwaka mmoja kabla ya Salah kucheza mechi yake ya kimataifa na walimaliza washindi wa pili katika michuano ya mwaka 2017 na 2021.

Alifunga penalti ya dakika za lala salama Jumapili iliyopita na kusaidia Misri kutoka sare ya mabao 2-2 na Msumbiji ili kuepuka kichapo cha aibu cha ufunguzi mapema kwenye michuano hiyo.

Salah ana imani kuwa atashinda Afcon "hivi karibuni au baadaye".

"Ningependa kushinda, kabisa," alisema. "Itatokea kwa namna fulani - ndivyo ninavyoamini. Chochote ninachoamini, ninafanikiwa - mapema au baadaye, kitatokea.

"Nimeshinda kila linalowezekana lakini hii, bado. Kila mtu anajua nini maana ya mchezaji yeyote kushinda Kombe la Afrika.

"Wachezaji wana ari kubwa ya kushinda michuano hiyo. Ninaamini kwamba, kwa bidii, kila kitu kinawezekana, hivyo tunahitaji kushinda mchezo mmoja tu ili tufuzu na tuondoke."

# NINA MBINU YA KUFUNGA KILA MCHEZO – ZWANE



**KORHOGO,** Ivory Coast

NYOTA wa Afrika Kusini, Themba Zwane, amesema mbinu yake aliyojiwekea kwenye kila mchezo inamhusisha kupata bao.

Zwane, ambaye alifunga mabao mawili katika ushindi mnono wa mabao 4-0 wa Afrika Kusini dhidi ya Namibia Jumapili usiku, alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa mechi kwenye mtananage huo uliopigwa Uwanja wa Amadou Gon Coulibaly hapa Korhogo.

"Kila mechi naenda kwa kujiamini na kufunga mabao. Wachezaji wanaoshambulia wanahitaji kufunga, na nina furaha kuwa nimefunga na kupokea tuzo hii.

"Ina maana kubwa kupata tuzo ya mchezaji bora wa mechi na furaha kubwa kupata ushindi leo (juzi)," alisema Zwane.

Akiwazungumzia wapinzani wake wajao, Zwane alisema watafanya uchambuzi wa kina kuhusu Tunisia na kupanga namna ya kuwakabili wababe hao wa Afrika Kaskazini.

"Tunajua kuwa bado haijaisha. Itakuwa ngumu dhidi ya Tunisia. Tutazichambua vizuri na tuje na mpango bora.

"Tunajua kwamba hakika tunahitaji kushinda ili tufuzu," alisema mchezaji huyo wa klabu ya Mamelodi Sundowns.

Ushindi huo unaipeleka Afrika Kusini hadi nafasi ya pili nyuma ya Mali kabla ya mechi yao muhimu dhidi ya Tunisiaa Jumatano.

Tunisia ipo mkiani mwa kundi ikiwa na pointi moja.

# Kocha wa Morocco akubali kubeba lawama DR Congo

**SAN-PEDRO,** Ivory Coast

KOCHA wa Morocco, Walid Regragui, amesema lawama zote amezibeba yeye kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya DR Congo Jumapili kwenye mechi yao ya Kundi F.

"Tulianza mechi vizuri. Tulijitengenezea mazingira, lakini tukarudi nyuma na kuwaruhusu kurejea mchezoni," alisema.

"Mabadiliko ya kuleta hali mpya zaidi hayakufaulu. Hatukujua jinsi ya kusimamia mechi inavyotakiwa, nawajibika kwa mechi hii," alikiri kocha huyo.

Regragui aliongeza kuwa wangeweza kuwa bora kimbinu katika mtazamo wao.

"Tuliacha nafasi nyingi sana kati ya mistari yetu. Kiufundi tunapaswa kuwa bora. Labda tuliiheshimu sana Congo.

"Walikuwa timu ngumu zaidi kwenye kundi. Walikuwa na motisha na kulipiza kisasi. Walikuwa hatari na hatua yao ilistahili," aliongeza.

Morocco imesalia kileleni mwa Kundi F ikiwa na pointi nne kabla ya mechi yao ya mwisho ya kundi hilo dhidi ya Zambia.





# Kocha Zambia asikitishwa na sare

**SAN-PEDRO,** Ivory Coast

KOCHA Mkuu wa Zambia, Avram Grant amesikitishwa na sare yao dhidi ya Tanzania kwenye mchezo wa Jumapili wa michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), hapa San-Pedro.

Vijana wa Grant walifunga bao dakika za majeruhi kwenye mchezo huo, lakini hakufurahishwa na timu yake licha ya kukiri jinsi Tanzania ilivyokuwa imara kwenye mchezo huo.

"Ni matokeo ya kukatisha tamaa. Tulijua isingekuwa mechi rahisi baada ya kutazama mechi ya Tanzania dhidi ya Morocco. Ni kweli kwamba tulianza vizuri pia, lakini tuliruhusu bao haraka na hiyo ilibadilisha mbinu zetu hasa baada ya kadi nyekundu," alisema.

Zambia ambayo ilibeba kombe hilo mwaka 2021 ilicheza na wachezaji 10 kwa sehemu kubwa ya mchezo huo na kocha huyo anaamini hiyo ilikuwa na athari kwao.

"Ni ngumu kucheza na wachezaji kumi. Lakini nimefurahishwa na majibu ya vijana. Walitoa kila kitu kurudi kwenye mchezo."

Zambia katika mchezo wa mwisho wa Kundi F itacheza na Morocco.

Na Grant anaamini timu yake ina nafasi ya kufanya vizuri kwenye mchezo huo dhidi ya 'Simba wa Atlas'.

"Tayari tunajua Morocco ni timu kubwa, lakini hatuwaogopi. Tutacheza nao na natumaini tutafanya vizuri. Itabidi tuoneshe kiwanho cha juu."

"Hicho ndicho tunachojaribu kufanya kila siku, kuwa bora. Na katika ngazi zote. Tangu nimekuwa nikifundisha timu hii, tumepiga hatua katika maeneo kadhaa, lakini lazima tuendelee. Hata unapokuwa bingwa, lazima uendelee kuboresha timu."

HABARI MICHEZO

# Wasanii watakiwa kuwa mfano bora kwenye Elimu ya Fedha

**Na Peter Haule (WF),** MOROGORO

WASANII wanaoshiriki kampeni ya kutoa elimu ya fedha kwa wananchi kutoka Shirika la Kijamii linalojishughulisha na utoaji wa Elimu ya Uraia (TACCI), lililopata semina ya elimu hiyo, wametakiwa kuwa mfano kwa jamii kwa kuzingatia sheria na kanuni za uendeshaji wa shughuli hizo.

Hayo yameelezwa mkoani Morogoro na Kamishna Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Janeth Hiza, wakati akifunga Mafunzo ya Elimu ya Fedha kwa Wasanii, yaliolenga kutoa elimu hiyo kwa njia bunifu ya sanaa.

"Wizara ya Fedha tunajipanga kwenda vijijini kutoa elimu ya fedha, kwa kuwatumia wasanii wa ngoma, nyimbo na maigizo na tunatamani kuona wananchi wengi zaidi wanafikiwa kwa njia rahisi lakini yenye ufanisi" alisema.

Amewataka wasanii kuendelea kubuni sanaa zinazoelimisha jamii kwa kuwa kazi za sanaa zinamvuto na hazichoshi kuzisikiliza na kuzitazama, hivyo zikitumiwa kwa malengo chanya zitatoa mchango mkubwa katika kusukuma gurudumu la maendeleo nchini.

Akizungumza kwa niaba ya wasanii wa Shirika la Kijamii linalojishughulisha na utoaji wa Elimu ya Uraia (TACCI), Mtaalam wa Sanaa za Jukwaani, Harrison Kisaka, alisema kuwa elimu waliyoipata mwanzo ilikuwa na lengo la kuisaidia jamii hasa vijijini, lakini imekuwa msaada mkubwa kwa wajumbe wote wa mafunzo hayo, hivyo akaahidi kuwa watakuwa chachu ya uelewa wa elimu hiyo kwa jamii inayowazunguka.

# KOCHA YANGA AMVULIA KOFIA KIPA WA SIMBA U20 KUWANYIMA USHINDI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa kikosi cha Yanga chini ya miaka 20, ambacho juzi kilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Simba, Vicent Barnabas, amesema hawakurudia kile walichokifanya mwezi mmoja uliopita kwa kushinda mabao 4-0, kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na kipa, Almas Adam.

Akizungumza baada ya mechi ya Ligi ya Vijana chini ya miaka hiyo iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, kocha huyo ambaye ni winga wa zamani wa Mtibwa Sugar na Yanga, alisema kipa wa Simba ndiye aliyewanyima ushindi, lakini hawakuzidiwa mahali popote, vinginevyo vijana wake wangeweza kupata ushindi wa mabao mengi zaidi.

"Mechi imeisha kwa bao 1-1, lakini wachezaji wangu wamecheza kwa kiwango kikubwa sana kitu ambacho siku zote tunawasisitiza, ni kwa vile tu matokeo yamegoma, lakini walivyopambana hata watu walioangalia kwenye televisheni nyumbani na waliokuja uwanjani wameona, ukimtaja nyota wa mchezo wa mechi yetu ni kipa wa Simba, kijana amejitahidi sana, ameonesha uwezo mkubwa, ametunyima sana mabao leo, nimpe tu hongera yake, vinginevyo tulikuwa tunashinda idadi kama ile ya mwanzo au zaidi leo," alisema kocha huyo.

**Hata hivyo, alisema wameimaliza mechi hiyo kwa sare na sasa wanajiandaa na mechi dhidi ya Coastal, itakayochezwa Februari 7, mwaka huu wakisahau kabisa matokeo ya mechi ya juzi.**

Kocha wa kikosi cha Simba chini ya miaka 20, Mohamed Mrisho, alisema vijana wake wamepambana na kuwazuia wa Yanga ambao walikuja kwa lengo la kutaka kushinda idadi kubwa ya mabao kama ilivyokuwa mwanzo.

"Tuliwasoma kwenye mechi ya kwanza, tukarekebisha makosa yetu, na ilikuwa kidogo tushinde mechi hii," alisema kocha huyo.

Simba ilitangulia dakika ya saba kwa bao la Juma Yusuph, kabla ya Willson Christopha kusawazisha dakika ya 39.

Desemba 22, mwaka jana, Yanga ilipata ushindi wa mabao 4-0 katika uwanja huo, kwenye mfululizo wa mechi za Ligi ya Vijana inayoendelea.

**INONGA KAZINI...**



Beki wa Kati wa DR Congo, Henock Inonga Baka, akimiliki mpira dhidi ya beki wa kulia wa Morocco, Achraf Hakimi, kwenye mechi ya Kundi F ya Fainali za Mataifa ya Afrika iliyopigwa nchini Ivory Coast juzi na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Taifa Stars yaapa kufa na DRC

INATOKA UK. 24

sha kuumia kwa sare hiyo, lakini aliwapongeza wachezaji wa timu ya Tanzania kwa kupambana hadi dakika ya mwisho.

"Hii imeuma, nimejisikia vizuri kwa sehemu kubwa ya mchezo leo, lakini ndio hivyo. Tunaendelea kujitafuta, tutajipata tu. Asante vijana wetu Taifa Stars kwa mapambano, haina kushika tama," alisema Naibu Waziri huyo.

Ilibaki dakika mbili tu Stars iweke rekodi ya kushinda mechi ya kwanza ya AFCON, tangu kuanzishwa kwake.

Aliyezima ndoto hizo ni straika anayeichezea Ligi ya England katika Klabu ya Leicester City, Patson Daka, aliyepachika bao la kusawazisha dakika ya 88 kwa kichwa, akiunganisha mpira wa kona iliyopigwa na Clatous Chama anayechezea Klabu ya Simba ya hapa nchini.

Awali, Stars ilitangulia kupata bao dakika ya 11 lililowekwa wavuni na Simon Msuva, aliyefunga kwa shuti kali baada ya kazi nzuri iliyofanywa na nahodha, Mbwana Samatta.

Ilikuwa ni sare ya kwanza kwa Stars baada ya miaka 44 kwenye hatua za fainali ambapo imetinga mara tatu.

Mara ya mwisho Stars kutoka sare kwenye Fainali za AFCON ilikuwa Machi 15, 1980 ilipotinga kwa mara ya kwanza na fainali zake kuchezwa nchini Nigeria, ikitoka sare kama ya juzi ya bao 1-1 dhidi ya Ivory Coast.

Ivory Coast ilianza kupata bao dakika ya saba lililofungwa na Michel Goba, kabla ya Stars kusawazisha dakika ya 57 kwa mpira uliowekwa wavuni na Thuwein Ally.

Mara ya pili ilipotinga Fainali za AFCON 2019 zilizochezwa nchini Misri, Stars ilipoteza mechi zake zote tatu za Kundi C.

# Benchikha apigilia nyundo

INATOKA UK. 24

klabu.

Miongoni mwa wachezaji wapya waliotambulishwa ndani ya Simba ni Babacar Sarr, Pa Omar Jobe, Fredy Michael, Saleh Karabaka, Ladack Chasambi na Edwin Balua.

Katika hatua nyingine Kocha Benchikha anatarajia kutua nchini muda wowote akitokea kwao Algeria kwenye mapumziko ya mafupi na kurejea katika majukumu ya kazi yake ya kuimarisha timu yake kwa ajili ya mzunguko wa pili wa ligi kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema kuna baadhi ya nyota wa kigeni hasa wachezaji wapya waliosajiliwa dirisha dogo wataanza kuwasili tayari kuanza rasmi mazoezi keshokutwa, Alhamisi katika Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju.

Alisema Benchikha anarejea kwa ari mpya kwa ajili ya kukinoa kikosi cha timu yao kwa wachezaji wote kasoro wale ambao wako kwenye majukumu ya timu za taifa zinazoshiriki fainali za Mataifa ya Afrika, AFCON.

# Michezo

Jumanne Januari 23, 2024

Nipashe




Salah aiacha Misri Afcon

UKURASA 21

TULIA...



Mfungaji wa bao la Taifa Stars, Simon Msuva, akimiliki mpira dhidi ya straika wa Zambia, Lameck Banda, kwenye mechi ya Kundi F ya Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), iliyopigwa Uwanja wa Laurent Pokou, San-Pedro nchini Ivory Coast juzi usiku na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# TAIFA STARS YAAPA KUFA NA DR CONGO

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Kocha asema hiyo ni mechi ya maamuzi na hakuna timu ndogo, atoa sababu sare...

KAIMU Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Hemed Morocco, amesema watahakikisha wanafanya kila njia ili kupata ushindi kwenye mechi ya mwisho ya Kundi F dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kesho, Jumatano ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele.

**Morocco alisema hayo nchini Ivory Coast baada ya mechi ya Stars dhidi ya Zambia iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Laurent Pokou uliopo San-Pedro, na kumalizika kwa kwa sare ya bao 1-1.**

Kocha huyo ambaye amechukua mikoba ya Adel Amrouche, aliyefungiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) kutokaa benchini mechi nane, na kusimamishwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kwa kile kilichodaiwa kutoa maneno ya kichochezi, alisema katika mechi ya juzi wachezaji wake walijitahidi kwa kila hali na kupambana, lakini bahati tu haikuwa yao.

Hata hivyo, aliwahakikishia Watanzania kuwa wachezaji wa Stars watapambana pia kwenye mechi ya mwisho dhidi ya DR Congo ili kupata ushindi kwa sababu itakuwa ni ya maamuzi na watakuwa wamesharekebisha makosa yaliyoonekana katika mechi iliyopita.

"Nashukuru wachezaji, kila mmoja amejaribu kupambana kwa uwezo wake, mechi hizi zote zipo kwenye 'levo' moja, huwezi kusema timu hii nzuri kuliko hii, hakuna mdogo, tutajipanga kujaribu kurekebisha pale ambapo panaonekana kuna matatizo, nafikiri tutakuwa vizuri kwenye mechi dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, nafasi ipo, na naahidi tutakuwa vizuri zaidi kwenye mechi dhidi ya Wakongomani," alisema kocha huyo.

Alisema wangeweza kuimaliza mechi mapema baada ya mchezaji wa timu hiyo, Roderick Kabwe kuonyeshwa kadi nyekundu, lakini wachezaji wake wakakosa umakini kwa kuonekana kujiamini zaidi.

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamisi Mwinjuma maarufu Mwana FA, mbali na kuonye-

INAENDELEA UK. 23

# Benchikha apigilia nyundo mikataba wachezaji Simba

**Na Saada Akida**

VIONGOZI wa Simba wameamua kukubaliana na Kocha Abdelhak Benchikha kwa kuweka vipengele vigumu kwenye mikataba ya wachezaji, hususan ni suala la nidhamu ndani na nje ya uwanja hasa kwa wachezaji wapya waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo lililofungwa wiki iliyopita na watakaosajiliwa msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema kwa sasa hawatakuwa wapole kwa mchezaji yeyote ndani ya klabu hiyo atakayeonesha nidhamu mbovu ikiwamo kwenda tofauti na kile kilichowekwa na kocha wao, Benchikha na watakaoenda tofauti na vipengele vya mkataba .

"Viongozi hatutakuwa tayari kuona mchezaji anaenda kinyume na vipengele vya makubaliano, tunaungana na benchi la ufundi linaloongozwa na Benchikha kutovumilia mtu ambaye anajiona yeye ni mkubwa kuliko timu, hata ukiwa kipenzi cha mashabiki usipokuwa na nidhamu hatuwezi kumvumilia," alisema Mtendaji huyo.

Inasemekana kuwa kocha Benchika ndiye aliyewashauri viongozi wa Simba kuweka baadhi ya vipengele hivyo kwenye mikataba ya wachezaji baada ya kukuta nidhamu mbovu kwa baadhi ya wachezaji wa timu hiyo, na viongozi wakaridhia.

Ikumbukwe kiungo wao, Clatous Chama, amesimamishwa na kupelekwa kwenye kamati ya nidhamu, lakini pia Mosses Phiri kabla ya kutemwa aliondolewa dakika za mwisho kwenye kikosi katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco waliocheza hapa nchini baada ya kuchelewa muda wa chakula.

Taarifa zinaeleza kuwa Benchikha alipofika nchini aliweka mikakati yake kwa wachezaji wanapokuwa kambini ikiwamo suala la kuvaa sare, kutochelewa muda wa kula na mazoezi, na kwamba hata wachezaji wapya waliosajiliwa kipindi cha dirisha dogo wamekutana na kitu hiki huku wakiambiwa hakuna mchezaji bora ndani ya timu hiyo zaidi ya

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >